

**AMORIM AFURAHISHWA MZOZO WA HOJLUND, AMAD**

UKURASA 22

**DK. MPANGO** ahimiza vyuo vikuu kuweka katika utafiti

UKURASA 2

**TRA** yazindua boti kupambana na wakwepa kodi

UKURASA 4

**WAZIRI** Ndumbaro anyooshea kidole viongozi wa dini mmomonyoko maadili

UKURASA 5

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumamosi Desemba 14, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581890
epaper.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

# Kilio upungufu maji chatikisa

**BAADHI** wadai kupata yakiwa machafu, DAWASA yatoa sababu... *Endelea ukurasa wa 2*



## Lissu asema hana mrithi nafasi yake CHADEMA

UKURASA 3

## WB yavutiwa na utekelezaji mradi wa SGR

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA KUFA NA TP MAZEMBE LEO UK. 24 **KATUNI** UK. 6

HABARI KITAIFA

# Mpango ahimiza vyuo kuwekeza katika utafiti

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema ili kuinua viwango vya utafiti, vyuo nchini vinapaswa kuwekeza kwenye eneo hilo hususani katika sayansi na teknolojia na kuhimiza ubunifu katika ufundishaji na ujifunzaji.

Aliyasema hayo jana katika Mahafali ya 27 ya Chuo Kikuu cha Iringa (UoI) yaliyofanyika katika viwanja vya chuo hicho mkoani Iringa.

Dk. Mpango alitoa wito kwa vyuo vikuu na taasisi zingine za elimu ya juu kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi ili kufundisha masomo na ujuzi muhimu unaokosekana nchini.

Kadhalika, aliwataka kufundisha ujuzi wenye wataalamu wachache kama vile madaktari bobezi wa upasuaji wa neva (neurosurgeon) na upandikizaji wa uroto (none-marrow transplant).

Maeneo mengine, kwa mujibu wa Dk Mpango ni upandikizaji wa figo, uhandisi wa roboti, fizikia ya nyuklia, matumizi ya akili mnemba na teknolojia.

Makamu wa Rais pia alitoa wito kwa sekta binafsi kuunga mkono jitihada hizo kwa kuendelea kushirikiana na vyuo vya elimu ya juu kwa kufadhili utafiti kwa wanafunzi wa fani mbalimbali.

Pia alisisitiza kushirikiana na vyuo vya elimu ya juu kwa kutoa nafasi za mafunzo kwa vitendo na mafunzo kazini.

Dk. Mpango alisisitiza umuhimu wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi ya elimu ya juu.

Alisema uwekezaji katika mifumo ya TEHAMA utawezesha ufundishaji wa baadhi ya masomo kwa njia ya mtandao na hivyo kuongeza idadi ya Watanzania watakaopata elimu ya juu.

Makamu wa Rais alisema ufundishaji kwa njia ya mtandao utapunguza changamoto ya uhaba wa walimu ambapo mmoja anaweza kuwafikia wanafunzi wengi kwa wakati mmoja.

Aliwasihi wahitimu kutumia fursa mbalimbali zilizoko nchini kama vile sekta za kilimo, biashara, ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba, nishati jadidifu, matumizi ya teknolojia za kidijitali na TEHAMA, unenepeshaji wa mifugo, ufugaji wa nyuki, biashara na viwanda vidogo vidogo ili kujipatia mitaji.

Dk. Mpango aliwatahadharisha wahitimu kuhusu tabia ya kupenda mafanikio ya haraka pasipo kufanya kazi kwa bidii.

"Ninawasihi kupenda kufanya kazi, kuepuka njia rahisi, kuwa waadilifu na waaminifu. Ninapongeza jitihada za Kituo cha Ujasiriamali na Ubunifu na matamizi ya Kiota (Kiota Innovation Hub) ya Chuo Kikuu cha Iringa kwa kutoa mafunzo ya ubunifu na ujasiriamali kwa wanafunzi na wajasiriamali," alisema.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***




Makamu wa Rais Dk Philip Mpango akipokea tuzo maalum ya utunzaji mazingira iliyotolewa na Chuo Kikuu cha Iringa katika mahafali ya chuo hicho yaliyofanyika jana mkoani Iringa, anayekabidhi tuzo ni Mkuu wa Chuo Kikuu Cha Iringa, Mkuu wa Majeshi Mstaafu Jenerali Venance Mabeyo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Kilio upungufu wa maji Dar chatikisa

**Na Jenifer Gilla**

WAKATI wananchi katika maeneo mbalimbali Dar es Salaam wakilalamikia kukosa huduma ya majisafi takribani miezi miwili, wanaopata baadhi wanasema yamekuwa yakitoka machafu.

Maeneo ambayo yanalalamikiwa kuwa na ukosefu wa maji kwa muda huo ni Mbezi Juu, Kinyerezi, Tabata Segerea, Kiluvya, Goba na Kimara, huku yanayopata lakini hutoka machafu ni pamoja na eneo la Mwenge.

Baadhi ya wananchi wakizungumza na mwandishi wa habari hii, walikiri kupata changamoto hizo za maji katika maeneo yao.

Mkazi wa Mtaa wa Zimbili, Tabata Kinyerezi, Rhoda Alphonce, alisema wana changamoto kubwa ya maji kwa sababu kwa sasa ni takriban miezi miwili hayatoki.

Alisema licha ya kuwasilisha malalamiko yao Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (DAWASA) lakini mpaka sasa kero hiyo haijatatuliwa na hawafahamu sababu.

"Wale wasoma mita tuliwazuia kuja kusoma ankara za maji kwa sababu kwa miezi miwili hupati maji. Tunaishi kwa kununua maji kwenye magari," alisema.

Victor Benard, mkazi wa Goba eneo la Mji Mpya, alisema katika maeneo yao hukosa huduma ya maji hata miezi mitatu.

Mkazi wa Mwenge, Mary James, alisema pamoja na kupata huduma ya maji, lakini yamekuwa yakitoka machafu na wakati mwingine yakiambatana na harufu na hali hiyo imekuwa ikijirudia kwa muda mrefu sasa.

"Unaletewa ankara ya maji ya Sh. 40,000 halafu ukiangalia ndani ya huo mwezi umelazimika kumwaga maji mengi kutokana na kuwa machafu na wakati mwingine hutoka yakiwa na tope unajiuliza hii ni huduma ya majisafi ama majitaka," alisema.

Mary aliiomba mamlaka husika kuongeza umakini kwa kuhakikisha huduma wanazotoa kwa wananchi hazigeuki kuwa kero kwao hasa hizo zinazomlazimisha mtumiaji kulipia.

Kauli hiyo imeungwa mkono na Magdalena Mushi, mkazi wa Tabata Barakuda, ambaye analalamika kuwa tangu utaratibu wa kutoka kwa maji kubadilika na kuwa mara moja kwa wiki, wamekuwa wakikumbana na tatizo la maji machafu kutoka bombani.

"Kuna siku yanatoka yakiwa na rangi ya udongo, siku nyingine rangi nyeusi ambayo huambatana na harufu mbaya. Inatulazimu kuyatumia baada ya kuyawekea dawa," alisema.

Jumanne ya wiki hii (Desemba 10), DAWASA ilitaarifu kuwa wananchi wanaohudumiwa na mtambo wa Ruvu Juu watakosa huduma kwa saa 24 kuanzia Desemba 10 hadi 11, mwaka huu, kutokana na matengenezo ya bomba kubwa la inchi 40 linalosambaza maji katika maeneo hayo.

Ilitaja maeneo yatakayoathirika kuwa ni Chalinze, Kijini cha Mboga, Ruvu Darajani, Ruvu JKT, Vigwaza, Mlandizi, Mbwawa, Visiga, Maili 35, Misugusugu, Kongowe, Soga, Miembe Saba, Kwa Mfipa, Mwendapole, Tanita, Kwa Mathias, Kwa Mbonde, Picha ya Ndege, Lulanzi na Kibaha.

Maeneo mengine ni Kiluvya, Kibamba, Mbezi, Magari Saba, Mbezi Inn, Mbezi, Kimara, Tabata, Segere, Kinyerezi, Kisukuru, Bonyokwa, Msigani, Maramba Mawili, Kimara B, Kimara Korogwe, Bucha, Baruti, Ubungo, Magomeni, Ukonga, Uwanja wa Ndege, Kiwalani, Vingunguti, Gongo la Mboto, Pugu na Kisarawe.

Mkazi wa Kiluvya, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, Ally Mohamed, alisema tatizo la maji katika eneo hilo lilianza tangu Desemba 7, mwaka huu na si Desemba 10 kama mamlaka hiyo ilivyoutaarifu umma.

Alisema kwa sasa wanatumia maji ya chumvi pekee ambayo pia, gharama zake zimepanda kutoka Sh. 15,000 kwa lita 1,000 na sasa imefikia Sh.25000.

"Niliagiza maji tangu juzi asubuhi, lakini yalifika jana, kwa hiyo nikalazimika kununua maji ya dukani ya lita 18 madumu matatu kwa Sh. 21,000 ya kutumia nyumbani," alisema Miriam Gregory, mkazi wa Kimara.

Mkazi wa Mbezi Juu, Ashura Said, alisema upatikanaji wa maji katika eneo lao umekuwa wa shida ,kwani kabla ya matengenezo hayo yamekuwa yakitoka mara moja kila baada ya siku kumi.

**KAULI YA DAWASA**

Alipotafutwa na mwandishi wa gazeti hili kuhusiana na upatikanaji wa maji katika eneo moja la Kibamba, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa DAWASA, Everlasting Lyaro, alisema ni mzuri isipokuwa kwasasa umeathiriwa na maboresho yanayoendelea katika Mtambo wa Ruvu Juu.

Alisema marekebisho hayo yatakapokamilika hali ya upatikanaji wa maji itatengemaa kata zote tano za kihuduma ambazo ni Kiluvya, Mbezi, Kibamba, Msigani na Kwembe.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Lissu asema hana mrithi nafasi yake CHADEMA

**Na Restuta James**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ametangaza kuwa hana mgombea wa kurithi nafasi yake ndani ya chama hicho.

Amesema yuko tayari kufanya kazi na yeyote ikiwa yeye atachaguliwa kuwa mwenyekiti.

Wakati Lissu anasema hayo, Kamati Kuu ya CHADEMA imetangaza leo kukutana Dar es Salaam, huku agenda zake zikiwa ni pamoja na usaili na uteuzi wa wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi Kanda za Kaskazini na Kati na maandalizi ya Mkutano Mkuu wa uchaguzi wa chama ngazi ya taifa.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii jana, Lissu alisema atafanya kazi na Makamu Mwenyekiti yeyote atakayechaguliwa na kuwataka wajumbe wamchague mtu mwadilifu.

Kauli hiyo ameitoa ikiwa ni siku moja baada ya kutangaza kugombea uenyekiti wa taifa wa CHADEMA ambayo kwa sasa inashikiliwa na Freeman Mbowe.

"Yeyote ambaye atajitokeza na hana mawaa, mimi nitakwenda naye, hatuhitaji watu wenye mawaa, lakini sio mimi nitakayechagua Makamu Mwenyekiti, itabidi ajitokeze. Akichaguliwa mwenye mawaa itakuwa shida," alisema Lissu.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Itifaki na Mambo ya Nje ya chama hicho, John Mrema, kwa vyombo vya habari, ilisema kikao hicho kitaongozwa na Mwenyekiti Mbowe.

Wakati Kamati Kuu ikijifungia, taarifa za ndani ya chama hicho zinasema uchaguzi wa viongozi wa taifa CHADEMA utafanyika mwezi ujao.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, alisema mwezi na tarehe ya uchaguzi itatangazwa Jumatatu ijayo.

Kuhusu idadi ya makada ambao wamejitokeza kuwania uenyekiti na makamu mwenyekiti, Mnyika alisema wote wanaojitokeza anawasilisha majina kwenye Kamati Kuu, ambayo inatoa ruhusa ya kuyatangaza au kutotangaza.

"Kwa wale ambao wameshajitangaza, ninaweza kuthibitisha kwamba, nimepokea barua zao. Nimepokea ya (barua ya) Mheshimiwa Lissu," alisema.

Taarifa za ndani zinaeleza kuwa baadhi ya makada ambao wameonesha nia ya kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti ni Hezekiah Wenje, ambaye ni Mwenyekiti wa CHADEMA, Kanda ya Ziwa Victoria. Wenje pia aliwahi kuwa mbunge wa Nyamagana, jijini Mwanza.

Wengine wanaotajwa ni John Heche ambaye pia amewahi kuwa Mbunge wa Tarime na Mwenyekiti wa Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema.

Hata hivyo, Nipashe ilipomtafuta Lema ili kujua ikiwa atagombea nafasi hiyo, alisema kwa sasa amejiweka kando na siasa.

"Kwanza mimi sipo Tanzania, nipo Canada. Siasa nitafanya kwa kiasi kidogo sana, nimeamua nipumzike kidogo," alisema.

Wakati Lissu akitoa msimamo huo, makada wa CHADEMA wameendelea kunyukana mitandaoni.

Miongoni mwa makada wanaonyukana ni Meya wa zamani wa Ubungo ambaye pia ni Mwenyekiti wa CHADEMA, Kanda ya Pwani, Boniface Jacob, Martin Masese, aliyekuwa mgombea wa CHADEMA Mbarali, Liberatus Mwang'ombe, Yeriko Nyerere na makada wengine.

Kwa upande wake, Mwanaharakati Maria Sarungi, ametangaza kumuunga mkono Lissu, akieleza kuwa ni kiongozi makini anayetosha kukiongoza chama hicho katika kipindi hiki.

Juzi, Lissu alitangaza kumkabili Mbowe kwenye nafasi ya Uenyekiti wa CHADEMA, akiwa na agenda saba, ikiwamo ya kuisuka upya Katiba ya chama hicho, ili pamoja na mambo mengine kuweka ukomo wa uongozi wa chama, ubunge na udiwani wa viti maalum na kutengeneza mifumo ya kusimamia chaguzi huru na za haki.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Wafanyabiashara wadogo wakiendelea na shughuli zao pembeni mwa barabara inayoingia katika kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho Dar es Salaam jana. Uhaba wa maeneo ya kufanyia biashara umesababisha watapakae kila kona. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Rais Samia afanya uteuzi wa viongozi, Balozi Bana astaafu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemteua Majaba Magana kuwa Kamishna wa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dk. Moses Kusiluka, Magana anachukua nafasi ya Fatma Simba.

Taarifa hiyo ilisema kabla ya uteuzi huo, Magana alikuwa Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja Wakubwa, Benki ya Azania.

Aidha, taarifa hiyo ilisema Rais Samia amempangia Balozi Selestine Kakele kuwa Balozi wa Tanzania nchini Nigeria.

Balozi Kakele anachukua nafasi ya Balozi Dk. Benson Bana, ambaye amestaafu.

# WB yavutiwa utekelezaji mradi SGR, yachakata maombi mapya

Nipashe
WhatsApp Chaneli
Skani hapa kutembelea chaneli yetu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Dunia (WB) imeeleza kuvutiwa na hatua kubwa iliyofikiwa na serikali katika kutekeleza mradi wa kimkakati wa Reli ya Kisasa (SGR).

Kutokana na hatua hiyo, benki hiyo imeahidi kuweka mkono wake kusaidia ujenzi wa reli hiyo muhimu kwa kukuza biashara na ukuaji wa uchumi wa nchi.

Mkurugenzi wa WB Kanda ya Afrika anayesimamia Miundombinu, Wendy Hughes, aliyeko nchini kwa ziara ya kikazi, aliyasema hayo baada ya kufanya mazungumzo na mawaziri watatu wa kisekta.

Mawaziri hao ni Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, na Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega.

Hughes aliyeambatana na Mkurugenzi Mkazi wa WB Tanzania, Nathan Belete, na viongozi wengine waandamizi wa benki hiyo, alisema amesafiri kwa kutumia reli hiyo kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na kushangazwa na kiwango cha ubora wake wa viwango vya kimataifa.

Alisema WB inaendelea kuchakata maombi yaliyowasilishwa na serikali katika benki hiyo, na kwamba iko tayari kusaidia ujenzi wa reli hiyo ya kimkakati na kushauri pia, sekta binafsi ishirikishwe kikamilifu kuhakikisha kuwa malengo ya kuanzishwa kwa mradi huo yanafikiwa kwa ufanisi mkubwa.

Wakizungumza katika kikao hicho kuhusu mradi wa SGR, Waziri Nchemba na Prof. Mbarawa, waliishukuru Benki ya Dunia kwa kuamua kutoa fedha za kujenga mradi huo, ambao umefikia hatua mbalimbali za ujenzi na kuwa mfano barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Walisema mradi wa SGR unaogharimu zaidi ya Sh. trilioni 10 na ni muhimu katika kuimarisha biashara na usafirishaji wa abiria na mizigo ndani na katika nchi za ukanda wa Maziwa Makuu, ambapo biashara kati ya nchi hizo inatarajiwa kuongezeka na kusaidia kutatua tatizo la ajira kwa wananchi. Mkutano huo ambao uliwashirikisha wakuu wa taasisi katika sekta ya usafirishaji na ujenzi, ulikuwa na ajenda tatu zikiwamo ujenzi wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (BRT), Mradi wa Reli kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR) na namna ya kuimarisha ushirikiano katika kutekeleza miradi kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP).

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Mtoto afa kwa shoti ya umeme, dada anusurika

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MTOTO mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi minane, Martin Ndalu, amefariki dunia na mwingine kujeruhiwa baada ya kupigwa shoti baada ya kushika waya uliokuwa ukishikilia nguzo ya umeme katika Mtaa wa CG, Kata ya Kitete, Manispaa ya Tabora.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Richard Abwao, alisema tukio hilo lilitokea Jumanne saa 2:00 asubuhi.

Alisema mtoto huyo alimtoroka dada yake na kwenda nje na kushika waya uliokuwa umeshikilia nguzo ya umeme na ndipo alipopigwa shoti.

Alisema wakati dada yake akimvuta ili kumwokoa alipigwa shoti akaanguka.

"Walikimbizwa katika Hospitali ya Mkoa Kitete, lakini mtoto Martin alifariki dunia na dada yake anaendelea kupatiwa matibabu na hali yake inaendelea vizuri,"alisema Abwao.

Baba wa marehemu, Nyangi Martin, alisema siku ya tukio yeye pamoja na mke wake walikuwa shambani na waliwaacha watoto na dada yao.

Mashuhuda walisema, mara baada ya tukio hilo, wataalamu kutoka Shirika la umeme Tanzania (TANESCO), Mkoa wa Tabora walifika eneo la tukio na kutoa waya huo.



Meneja wa Kitengo cha Usimamizi wa Miradi, Kampuni ya Kawasaki Kiko ya Japan, Motohiro Handa akipima chai ya Tanzania juzi wilayani Mufindi kwa ajili ya kwenda kutengeneza mashine itakayoendana na uhalisia wa chai inayozalishwa nchini anayempiga picha ni Mkurugenzi wa Miradi ya Maendeleo wa Kampuni hiyo Hirofumi Suganuma nyuma yao aliyevaa shati jeupe ni Ofisa Kilimo Idara ya Maendeleo ya Mazao, Bahati Majaliwa, mwingine ni Mdau kutoka Taasisi ya Utafiti ya chai Tanzania (TRIT) **PICHA: HALFANI CHUSI**

# TRA yazindua boti ya doria kupambana na wakwepa kodi

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imezindua boti ya doria ambayo itatumika kupambana na magendo katika Ziwa Victoria na kukomesha vitendo vya ukwepaji kodi, ambavyo vimekuwa vikifanywa na watu wasioitakia mema Tanzania.

Akizindua boti hiyo jana mkoani Mwanza, Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Chande, alisema itasaidia kukomesha magendo yanayofanyika katika Ziwa Victoria.

Chande alisema kila Mtanzania kwa nafasi yake anapaswa kupambana na magendo kwa kuwa huumiza taifa zima na siyo TRA kama wengi wanavyodhani.

Kamishna Mkuu TRA, Yusuph Mwenda, alisema magendo yanayofanywa na baadhi ya watu wasiokuwa waaminifu yamekuwa yakichangia kuharibu uchumi wa nchi na kuhujumu biashara za wengine.

Kadhalika alisema huchochea uhalifu na kuharibu usalama wa nchi, hivyo boti hiyo ya doria iliyozinduliwa itakomesha vitendo hivyo.

Alisema boti hiyo itatumika kupambana na magendo na kuokoa mapato yaliyokuwa yanapotea kutokana na ukwepaji kodi kupitia bidhaa za magendo.

"Miongoni mwa magendo makubwa yanayoingia kupitia Ziwa Victoria ni vipodozi ambavyo mbali na kukwepa kodi, vimekuwa vikiharibu afya za wananchi na kazi yetu siyo tu kudhibiti tu mapato, tunaangalia afya za Watanzania," alisema.

Kamishna Mkuu Mwenda alisema walipakodi wanataka kuwapo na usawa katika kodi, hivyo kuzinduliwa kwa boti hiyo kunatekeleza matakwa yao ya kuzuia magendo ili kuwa na usawa wa biashara kwa kila mtu kulipa kodi.

"Usawa wa biashara unakosekana kwa kuwa unakuta mtu aliyeingiza bidhaa za magendo anaziuza kwa bei ya chini kuliko wenzake kwa sababu hajazilipia kodi, sasa tutahakikisha wote wanalipa kodi," alisema.

Alisema TRA itatoa motisha kwa yeyote atakayefichua watu wanaojihusisha na magendo au wanaokwepa kodi, kwa kuwa suala la motisha lipo kisheria.

Kamishna wa Forodha, Juma Hassan alisema boti hiyo ya kisasa ina mwendo wa kasi ya kutosha ya kupambana na magendo ambapo ni ya tatu kukamilika, huku ya nne ikiendelea na matengenezo.

Alisema ndani ya boti hiyo kuna vitanda vitatu pamoja na sehemu ya kupikia, ambayo itaiwezesha kukaa majini muda mrefu na matengenezo yake yanagharimu Sh. milioni 865.1.

Alisema boti za wazi ikiwamo iliyozinduliwa zimegharimu Sh. bilioni 1.6, sawa na Sh. milioni 530 kwa kila boti.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amina Makilagi, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, alisema wanashirikiana na TRA kuilinda boti hiyo.

Alisema Mkoa wa Mwanza unakusanya mapato mengi na hivyo kushika nafasi ya pili kwa makusanyo, jambo ambalo limewapa motisha baada ya kupatiwa zaidi ya Sh. trilioni tano za miradi ya maendeleo.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Msigwa ataka wanahabari kudumisha amani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MSEMAJI Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa amewataka waandishi wa habari nchini kutumia kalamu na kamera zao kuilinda Tanzania ili iendelee kuwa na amani, utulivu na maendeleo.

Msigwa ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukabidhiwa Ofisi na aliyekuwa Msemaji Mkuu wa Serikali, Thobias Makoba.

Alisema waandishi ni mhimili wa nne usio rasmi lakini wenye nguvu kubwa, ukitaka kukutikisa unatikisika na ukitaka kutuliza unakutuliza hivyo, waandishi wachague kutuliza nchi kwa kuwa inahitaji utulivu.

"Hii ni nchi yetu sote na sisi wote ni watanzania, nyinyi waandishi wenzangu wa habari ni watanzania na mnaishi Tanzania, hata kama kuna mwandishi wa habari sio mtanzania lakini anaishi Tanzania, wote tunajukumu la kuilinda Tanzania.

"Kazi yetu sisi waandishi wa habari ni kuilinda Tanzania kwa kalamu zetu, naomba kalamu zetu zitumike kuilinda nchi yetu, nchi yetu inataka amani, maendeleo, utulivu na haijazoea zogo wala vurugu tumkatae kwa nguvu zetu zote kwa kalamu zetu na kamera zetu yeyote anayetaka kutuvurugia tunu za taifa," alisema. Alisema baada ya sikukuu za mwisho wa mwaka atakutana na waandishi kwa ajili ya mazungumzo ili kuweka mikakati ya utendaji kazi.

Hata hivyo, alisema Desemba 19, mwaka huu, atatoa taarifa ya kwanza ya Msemaji Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.

"Utamaduni wa taarifa za Msemaji Mkuu wa Serikali ni muhimu sana, kuna mwingine anaweza kuchukulia poa, lakini niwaambie watanzania wakisikia msemaji mkuu wa serikali anazungumza wanasikiliza kwa sababu wanapata taarifa muhimu za serikali," alisema.

Balozi Makoba alisema ameondoka kwenye nafasi ya Usemaji akiwa amechangamka kwa kuwa kuna wakati wizara nne zilikuwa zinapigwa na anapaswa kutoa majibu kwa haraka.

"Nimeona uzalendo ndani ya waandishi, kuna wakati mtu asiyefahamu inakuwa kama vita anakwambia waandishi wenu hawa, mtu asiyeelewa hii sekta lakini tulipata shida hapa Kariakoo, kuna vitu ambayo sitasahau nilikaa siku tatu pale hatujaondoka na ni janga la kitaifa."

"Humu baadhi yenu tulikesha nao na wanauliza tufanye nini ili jamii iweze kutulia. Hakuna uzalendo kama huu kwa sababu mwandishi kalamu au picha yake inaweza kubomoa jamii lakini nimeona uzalendo wa hali ya juu,"alisema. Aliwaomba waandishi kuendelea kutumia kalamu zao kujenga taifa lenye mshikamano huku akimuahidi Rais Samia kuwa atatumia vipaji vyake kuhakikisha analitumikia taifa ili kuchochea maendeleo.

## Wahimiza elimu jinsia kupambana na ushoga

**Na Grace Mwakalinga**

POLISI Kata ya Kilungule, Manispaa ya Temeke, Dar es Salaam, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Rebecca Mgalama, amesema kuna muhimu wa kutolewa elimu ya jinsia kwa wanaume na vijana wa kiume, ili kukabiliana na ushoga na ulawiti unaoliandamana kundi hilo katika jamii.

Rebecca aliyasema hayo jana wakati akifunga mafunzo kwa waraghibishi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa kilichoko katika kata hiyo.

Alisema utafiti umebaini kuwanyima nafasi wanaume kushiriki katika kampeni hizo ambazo zimekuwa zikifanyika mara kwa mara nchini, ili kukabiliana na ukatili na udhalilishaji wanawake na watoto.

Alisema ni muhimu elimu ya jinsia iwafikie wanaume na vijana wa kiume ili kukabiliana na ushoga na ulawiti unaoliandamana kundi hilo katika jamii.

Kuhusu matukio ya ukatili wa kijinsia, Rebecca alisema, chanzo ni wazazi hususani wa wanawake kuwaamini ndugu wanaofika nyumbani kwao kwa kuwaruhusu kulala na watoto.

Alisema kwa kiasi kukubwa matukio ya ubakaji na ulawiti yanayoripotiwa kufanywa na ndugu wa karibu, ambao hulala na kuwa karibu na watoto.

"Tumefanya vizuri sana kutoa elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, lakini tumelisahau hili kundi la wanaume na vijana, matokeo yake tunayaona sasa, kuna wimbi kubwa na mashoga, tujitahidi kuokoa kizazi hiki hali ni mbaya," alisema Rebecca.

Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Hamis Mwanaupanga, alisema kata hiyo ya Kilungule inatarajia kuanzisha serikali ndogo kwa ajili ya kuwapatia ulinzi na usalama wa watoto katika eneo hilo.

Mwanaupanga alisema kuanzishwa kwa serikali hiyo ndogo kutazidisha mapambano dhidhi ya vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto baada ya kuanza kukithiri katika maeneo yao.

Alisema wameandaa vipengele vinne ambavyo ni haki ya mtoto, malezi na ulinzi na usalama wa mtoto.

"Tumeamua kuanzisha sheria ndogo kwa ajili ya kumlinda mtoto, kinachosubiriwa kwa sasa ni kupitisha katika baraza la madiwani ili zianze kutumika rasmi. Ninaamini zitatuongoza vizuri kusimamia masuala ya watoto kukabiliana na ukatili dhidi yao," alisema.

Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kilungule, Salma Gonga, alisema ni jukumu lao kuisaidia jamii kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Salma alisema katika kukabiliana na vitendo hivyo, wataendelea kutoa elimu kwa wanawake ambao ndio wamebeba jukumu la kutunza familia.

Ofisa Maendeleo wa Kata hiyo, Thereza Sinna, alisema wameanzisha klabu za kupinga ukatili wa kijinsia katika shule zote za Kilungule, kuwajengea uwezo wanafunzi kutambua athari za ukatili kwa watoto na namna ya kukabiliana nao.

Thereza alisema jukumu lake ni kupita kila shule kuzungumza nao kujua madhila wanayopitia na njia za kukabiliana nayo, utaratibu ambao anauona umesaidia kujitambua na kuongeza umakini wakati wa kwenda au kurudi shuleni.

# Ndumbaro anyooshea kidole viongozi dini kuhusu mmomonyoko wa maadili

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro, amewataka viongozi wa dini na wa kimila kuacha kuinyooshea serikali kidole kuwa inafanya nini pale maadili yanapomomonyoka ndani ya jamii ukiwamo ukatili.

Amesema suala hilo si la serikali pekee, bali ni la watu wote wakiwamo wao na jamii kwa ujumla.

Waziri Ndumbaro aliyasema hayo jana wakati akizindua Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal AID Campaign) inayotoa huduma bure za kisheria kwa siku tisa katika Halmashauri tisa za wilaya saba za Mkoa wa Morogoro.

Alisema suala la elimu ya maadili ni lazima lianzie nyumbani na taasisi za kidini, hivyo si jambo jema inapotokea serikali ikatupiwa lawama.

Waziri Ndumbaro alisema serikali haipendezwi na vitendo hivyo vya mmomonyoko wa maadili na ukatili wa kijinsia, ndio maana imekuwa ikifanya kila jitihada za kuhakikisha vinakoma.

Alisema kila mtu anawajibu wa kukemea na kuufuatilia mienendo ya watoto, kujua anayevifanya ili kulipwa anachostahili.

Akizungumzia kuhusu kampeni hiyo ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, Waziri huyo alisema kwa Mkoa wa Morogoro umelenga kumaliza migogoro ya ardhi pamoja na wakulima na wafugaji.

Alisema kampeni hiyo imelenga pia, kukomesha uharibifu wa mazingira kwa kuwa Morogoro ndio makao makuu ya Uhifadhi wa mazingira na asilimia 81 ya maji yanayokwenda kwenye bwawa la uzalishaji umeme la Mwalimu Nyerere yanatoka mkoa huo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Wakili Dunstan Kyobya alisema kampeni imejikita katika kutoa elimu ya kisheria kwa wananchi katika maeneo tofauti.

Aliyataja kuwa ni kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia, migogoro ya ardhi, mirathi, usuluhishi wa migogoro kwa njia mbadala na masuala yanayohusu haki za binadamu kwa ujumla.

Alisema lengo kuu ni kulinda na kukuza upatikanaji wa haki kwa wote kupitia huduma ya msaada wa kisheria nchini.

Baadhi ya wakazi wa Mkoa wa Morogoro, akiwamo Subira Mtandi, amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha mpango huo, kwani utasaidia kutatua changamoto iliyoko kwa wananchi.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi,Innocent Bashungwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhandisi Hamad Masauni wakipitia nyaraka wakati wa makabidhiano ya ofisi baada ya mabadiliko madogo ya baraza la mawaziri yaliyofanywa na Rais Dk.Samia Suluhu Hassan ambapo alimteua Innocent Bashungwa kuwa waziri wa wizara hiyo. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

# Watu 17 mbaroni tuhuma za mauaji, wizi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Singida limewatia mbaroni watu 17 wakituhumiwa kujihusisha na makosa mbalimbali ya jinai yakiwamo ya mauaji na wizi.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, ACP Hamis Mungwana, akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu operesheni zilizofanyika mwezi uliopita, alisema kati ya watuhumiwa hao watatu wamekamatwa kwa kosa la mauaji.

Alisema mtuhumiwa mmoja alikamatwa kwa kosa la kubaka, watano kwa wizi wa ng'ombe watano, mbuzi mmoja, viti viwili vya plastiki na watuhumiwa wawili walikamatwa kwa kosa la kukutwa na mali za wizi.

Alizitaja mali hizo kuwa ni robota 15 za nyavu za uvuvi haramu, mizani ya dukani, TV nchi 32 na pikipiki mbili zenye usajili MC 248 EKN aina ya Sinoray na MC 780 AVB aina ya Fekon.

Mungwana alisema mtuhumiwa mmoja alikamatwa kwa kosa la kuharibu mali ambapo alivunja vyungu na kuharibu mapipa ya pombe ya asili (mtukuru) ambayo ilikuwa ikiuzwa mnadani na watuhumiwa wawili walikamatwa na nyama ya swala na madini ambayo hayana kibali.

Kuhusu mafanikio ya kesi mahakamani, alisema washtakiwa 50 waliotuhumiwa kwa makosa mbalimbali walihukumiwa vifungo wakiwamo watatu waliohukumiwa kwenda jela baada ya kukutwa na hatia kwa kosa la kubaka.

Alisema washtakiwa watatu wa wizi walihukumiwa kwenda jela miaka saba kila mmoja, mshtakiwa mmoja alihukumiwa kwenda jela miaka nne kwa kosa la mauaji.

Alisema mmoja amehukumiwa jela miaka 30 kwa kupatikana na nyara za serikali, watatu wamehukumiwa miaka 30 kila mmoja kwa unyang'anyi wa silaha na mshtakiwa mmoja alihukumiwa kwenda jela miaka mitano kwa kukutwa na dawa za kulevya aina ya bhangi.

Alisema katika operesheni hiyo, madereva saba wamekamatwa na kufungiwa leseni za udereva kwa miezi mitatu kwa kosa la kuendesha magari yao kwa mwendokasi usioruhusiwa kisheria.

Aliwataja madereva hao kuwa ni Kelvin Shirima, dereva wa gari T 129 DRD aina ya Toyota Coaster, Ally Simba dereva wa basi la Kampuni ya Zuberi lenye namba za usajiri T 615 DUR, Athuman Kategire, dereva wa gari T 839 DPV aina ya Toyota Coaster.

Madereva wengine waliofungiwa ni Daniel Mhando wa gari T 275 DXW basi la Kampuni ya Travel Partner, Jumanne Hadi dereva wa gari T 618 DUR basi la Kampuni ya Kapricon, dereva wa basi la Asante Rabi lenye namba T 330 BAX na dereva wa gari T 712 DCL Shukru Mkotya.

Aliwataka wananchi kuchukua tahadhari wanapotumia vyombo vya moto kusafiri kwenda maeneo mbalimbali kwa ajili ya sikukuu na madereva waheshimu sheria za usalama barabarani.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji wakijitoa Yanga wanaweza kusonga mbele

**LEO** Yanga wana karata moja muhimu katika harakati zao za kutaka kucheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakapokuwa wageni wa TP Mazembe katika mchezo wa kundi A wa michuano hiyo.

Ni karata muhimu kutokana na ukweli kuwa mchezo huo umebeba matumaini ya wawakilishi hao wa Tanzania kwenye michuano hiyo ya vilabu barani Afrika.

Endapo Yanga ambayo imepoteza michezo yake miwili iliyopita, ikipoteza na mchezo wa leo utakaochezwa saa 10 jioni, itakuwa imejisafishia njia ya kuondolewa kwenye michuano hiyo.

Mpaka sasa ndio timu pekee kwenye kundi lake ikiwa haina pointi yoyote licha ya kucheza michezo miwili sawa na timu nyingine kwenye kundi hilo.

Matumaini pekee ya mashabiki na wanachama wa klabu hiyo yanabaki kwa wachezaji wa timu hiyo ambao ndio wanakazi kubwa ya kufanya ndani ya dakika 90 za mchezo huo.

Tunaamini Yanga wana timu nzuri na wachezaji wenye vipaji na uwezo mkubwa wa kusakata soka, na wanaweza wakatoa matokeo yoyote ndani ya dakika 90 za mchezo.

Hata hivyo wachezaji lazima watambue umuhimu wa mchezo huu wa leo kwa ajili ya mustakabali wa malengo yao ya kutaka kucheza kwa mara ya pili mfululizo hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Lakini pia bila ubishi ili kuweza kupata pointi tatu muhimu kwenye mchezo huu, ni lazima wachezaji wavuje jasho uwanjani na kujitoa muda wote wa mchezo kusaka alama tatu muhimu.

Kwenye soka hakuna kinachoshindikana, kama wachezaji wa Yanga watafuata maelekezo ya kocha wao na kuonesha juhudi muda wote wa mchezo, uwezekano wa kuvuna alama tatu upo.

Hakuna ubishi kuwa mchezo wa leo ni mgumu kwa pande zote, ugumu huo unatokana na uhitaji wa pointi tatu kwa kila timu kuweza kuweka hai matumaini yao ya kusonga mbele.

Yanga ambayo haina pointi yoyote, wanakutana na TP Mazembe yenye pointi moja waliyoivuna kwenye mchezo wao wa kwanza dhidi ya MC Alger huku timu zote zikipoteza kwenye michezo yao ya pili Yanga wakifungwa na Alger mabao 2-0 huku Mazembe wakikumbana na kipigo kutoka kwa Al Hilal.

Tunaishauri Yanga kuingia uwanjani kwa tahadhari wakisahau matokeo waliyoyapata mwaka jana dhidi ya wapinzani wao hao kwenye kombe la Shirikisho Afrika ambapo Yanga walipata ushindi nyumbani na ugenini.

Kama wachezaji wataamua kupambana kweli na kila mmoja kucheza kwenye kiwango chake cha juu, Yanga wana nafasi ya kupata ushindi kwenye mchezo huo.

Kwenye soka hakuna kinachoshindikana, ndani ya dakika 90 ni kupambana na kuwa makini kwa kila nafasi watakayoipata, tunaamini kutokana na ugumu wa mchezo huo kwa kila timu, hakutakuwa na nafasi nyingi za wazi za kuweza kufunga.

Safu ya ushambuliaji ya Yanga wanapaswa kuwa makini na kila nafasi watakayoipata,watumie nafasi hizo kupachika mabao na kuihakikishia timu ushindi.

Nipashe tunawatakia kila la heri Yanga tukiamini uwezo wa kushinda mchezo wa leo wanao na kuweka hai matumaini ya kuwa timu moja wapo watakaoingia hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Yanga, Simba bado mna nafasi kufuzu robo fainali ya CAF

**WAKATI** Yanga leo itajitupa kwenye Uwanja wa Lubumbashi, nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kucheza dhidi ya TP Mazembe kwenye mechi ya raundi ya tatu, Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, kesho Simba itakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kucheza dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia.

Mechi hii ni ya raundi ya tatu, Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi.

Kipigo cha mabao 2-0 ilichokipata Yanga dhidi ya MC Alger ya Algeria wiki iliyopita na mabao 2-1, ilichokipata Simba dhidi ya CS Conastantine kimewafanya baadhi ya mashabiki wa timu hizo waanze kukata tamaa ya kupita katika hatua ya makundi.

Baada ya mechi hizo, hata ukisoma kwenye mitandao ya kijamii, baadhi wanaonekana kukata tamaa kuwa inawezekana msimu huu timu zao zisiweze kupita hatua ya makundi na kwenda robo fainali.

Ni kwa sababu Yanga mpaka kufikia raundi ya pili haina pointi hata moja, lakini Simba pamoja na kwamba ina pointi tatu, lakini kiwango inachokionyesha kimeonekana kutowaridhisha baadhi ya mashabiki wake.

Niwaambie tu mashabiki wa soka nchini kuwa ni mapema mno kuzikatia tamaa timu hizo kwa sasa.

Iwapo Yanga itashinda mchezo wa leo, itakuwa imerudi kwenye reli na itakuwa imebakisha mechi mbili nyumbani na moja ugenini, hivyo chochote kinaweza kutokea.

Niwatoe wasiwasi wanachama na mashabiki wa timu hizi waendelee kuzisapoti timu zao waendelee kujitokeza viwanjani kama mechi inachezwa, Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa ajili ya kuwatia nguvu wachezaji.

Mara nyingi mashabiki wa soka nchini hawana tabia ya kwenda kujazana uwanjani kama timu zao zinafanya vibaya. Hii inaweza kufifisha juhudi za viongozi na wachezaji kutinga hatua ya robo fainali.

> **Ikumbukwe kuwa Simba ilipitia kipindi kigumu kama hicho, mfano tu msimu uliopita, ilitoka sare ya bao 1-1 nyumbani dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, suluhu ugenini dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, baadaye ikafungwa bao 1-0 ugenini dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco.**

Ikumbukwe kuwa Simba ilipitia kipindi kigumu kama hicho, mfano tu msimu uliopita, ilitoka sare ya bao 1-1 nyumbani dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, suluhu ugenini dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, baadaye ikafungwa bao 1-0 ugenini dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco.

Hapa utaona kuwa kwenye michezo mitatu ilikuwa haijashinda hata mchezo mmoja, lakini ikapambana na kushinda mabao 2-0 nyumbani dhidi ya Wydad Casablanca, kabla ya kulazimishwa suluhu kwa mara nyingine dhidi ya Asec Mimosas ugenini.

Hii inaonyesha kuwa Simba ilipita kwenye njia ngumu mno, kiasi kwamba mechi mbili za mwisho ililazimika kushinda zote, ikaifunga Jwaneng Galaxy mabao 6-0, na kutinga hatua hiyo.

Misimu mwili iliyopita kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba baada ya kupoteza michezo miwili mfululizo, ilionekana kama imeshatolewa kwenye kinyang'anyiro kwa kushika nafasi ya mwisho kwenye kundi, lakini ilishinda michezo miwili mfululizo dhidi ya Vipers ya Uganda na kurejesha matumaini, kabla ya mchezo wa mwisho kuikandamiza Horoya mabao 7-0, ikatinga kwa kishindo robo fainali. Mifano hii ni kuonyesha kuwa timu hizi zikikaa chini na kupiga hesabu zake vizuri, kuandaa mikakati ya ndani ya uwanja ya kiufundi ikichanganya na rasilimali watu ambao ni mashabiki wake kwa kuwahamasisha kujazana uwanjani kwenda kuzipa sapoti kama ilivyokuwa ikifanya Simba huko nyuma, ikipita mara kwa mara katika mazingira magumu, basi hakuna kitakachoshindikana.

# TIA yamwagiwa bil. 58/- ujenzi miundombinu

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Uhasibu (TIA), imepatiwa Sh. bilioni 58.1 kwa ajili ya kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo hususan ujenzi wa miundombinu ya kusomea na kufundishia.

Hayo yalisemwa juzi jijini Dar es Salaam na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Jenifer Omolo, wakati wa mahafali ya 22 ya taasisi hiyo.

Alipongeza uongozi na watumishi wa TIA kwa kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati huku akiwasisitiza kuhakikisha wanaweka mipango madhubuti ya kutunza miundombinu hiyo.

"Leo tunasherehekea mafanikio ya wahitimu 6,950 wa kampasi ya Dar es Salaam. Kama alivyoeleza Mtendaji Mkuu kwenye taarifa yake, wanawake ni 3,838 na wanaume ni 3,112. Nawapongeza sana wahitimu wanawake kwa bidii na mwamko mkubwa wa elimu," alisema.

Aidha, alisema katika dunia ya sasa inayobadilika kwa kasi, mifumo ya elimu inahitajika kubadilika ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira na aliwapongeza TIA kwa kuwa mstari wa mbele kupitia mpango wa vituo atamizi, unaowawezesha wanafunzi kujiajiri, kuajirika, na kuchangia uchumi wa taifa.

Aliwapongeza kwa kuwaendeleza wanafunzi wenye mawazo ya kibunifu ili kufanikisha malengo yao na kuongeza kuwa elimu na maarifa waliyopata ni nyenzo muhimu ya kuboresha maisha na kuchangia maendeleo ya taifa.

"Katika ulimwengu wa sasa wa teknolojia, tumieni ubunifu kutatua changamoto na fursa za kijamii na mitandao ya kijamii ni rasilimali yenye nguvu itumieni kwa njia chanya kama vile kujifunza, kujitangaza kibiashara, na kujipatia kipato," alisema.

Alisema ujasiriamali na uvumbuzi ni nguzo za mafanikio hivyo wachukue hatua na kutumia maarifa yao kwa faida ya jamii.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Prof. Wiliam Pallangyo, alisema Sh. bilioni 58.1 walizopewa zimewezesha ujenzi wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia katika kampasi za Mbeya, Mtwara, Mwanza, Kigoma, na Zanzibar.

Alisema katika mahafali hayo jumla ya 6,950 watatunukiwa cheti cha awali, stashahada, shahada, stashahada za uzamili, na shahada za uzamili kwenye fani za uhasibu, ununuzi na ugavi, usimamizi wa biashara, usimamizi wa rasilimali watu, masoko na uhusiano wa umma, uhasibu wa umma na fedha, na usimamizi wa miradi.

Prof. Pallangyo alisema wameanzisha kampasi ya nane mkoani Tanga na kwamba hiyo ni hatua muhimu inayotimiza dhamira ya TIA ya kufikisha huduma karibu na wananchi kupitia kampasi zake zilizopo kanda zote za Tanzania.

"Kampasi hizo zenye jumla ya wanachuo 31,084, zipo kimkakati katika mikoa ya Dar es Salaam, Singida, Mbeya Mtwara, Mwanza, Kigoma, Tanga na Zanzibar na kwamba kati yao, wanachuo 21,394 ni wa kampasi ya Dar es Salaam," alisema.

Alisema ongezeko hilo la wanachuo, limechangiwa na kuongezeka idadi ya wanufaika wa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Katika mwaka wa masomo 2024/2025, alisema wanachuo 12,263 wamenufaika na mkopo wenye thamani ya takribani Sh. bilioni 7.49 sawa na ongezeko la asilimia 35.9 kulinganisha na wanachuo 9,025 katika mwaka wa masomo 2023/24, waliopokea jumla ya Sh. bilioni 6.14.

Aliishukuru serikali kwa kuongeza idadi ya wanufaika na kiwango cha mkopo kwa wanachuo wa TIA na kuongeza kuwa katika kuhakikisha tunawaandaa wanachuo kukua kiujuzi na kitaaluma, kampasi ya Dar es Salaam imetoa mafunzo kwa wanachuo 6,000, yakilenga kuwajengea ujuzi kwa vitendo kuhusu ujasiriamali na ubunifu.

Mafunzo hayo, alisema yamechochea ubunifu mbalimbali na kwamba TIA imeendelea kushirikiana na vyuo na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kunufaisha wanachuo na watumishi wake, ili kuongeza ufanisi.

Alisema katika mwaka wa masomo 2023/2024, kampasi ya Dar es Salaam imefanikiwa kupeleka wanachuo wawili nchini Lithuania, kupitia mpango wa ubadilishanaji wanafunzi chini ya mradi wa Erasmus na mwanachuo mmoja aliiwakilisha Tanzania kwenye Bunge la Vijana la Jumuiya ya Madola.

Alisema katika kipindi cha Julai hadi Novemba, mwaka huu, kampasi ya Dar es Salaam, kupitia Kurugenzi ya Utafiti, Machapisho, na Ushauri wa Kitaalam, imefanikiwa kuendesha mafunzo kwa taasisi 120 na kuandaa Kongamano la Tatu la Kimataifa lililoshirikisha washiriki kutoka nchi za Urusi, Lithuania, Ghana, Eswatini, na Kenya.



Balozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa (kulia), Katibu Tawala wa mkoa wa Kigoma, Hassan Rugwa, Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, Mark Bryan Schreiner na Mkuu wa Mawasiliano wa UNFPA Dk.Warren Bright wakiwa na baadhi ya vifaa tiba vilivyotolewa msaada na shirika hilo, ikiwamo gari lilitolewa na Balozi huyo jijini Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya huduma za afya humo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali kuboresha huduma za dharura kupunguza vifo

**Na Beatrice Shayo**

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Mohamed Manguna, amesema serikali imeendelea kuboresha huduma za afya zikiwamo za dharura.

Kadhalika amesema wamewekа mikakati ya kina kwa ajili ya kujenga uwezo wa mfumo wa afya kwa kuidhinisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi.

Dk. Manguna aliyasema hayo wakati akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, katika hafla ya kufunga awamu ya kwanza ya mradi wa kuboresha huduma za dharura za Afya Tanzania (IMECT).

Mradi huo umefanyika kwa ushirikiano wa taasisi za umma na binafsi unaofadhiliwa na serikali ya Poland, taasisi ya huduma za afya za Aga Khan Tanzania na serikali.

Alisema hatua hizo zinalenga kuhakikisha huduma za dharura zinapatikana kwa urahisi, zenye ubora na kukidhi mahitaji ya wananchi kwa wakati.

Alisema mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 1.8 ni mfano bora wa mafanikio ya ushirikiano, ukileta pamoja serikali ya Tanzania, washirika wa kimataifa, na jamii za ndani katika jitihada za kuimarisha huduma za matibabu ya dharura kote nchini.

"Ninaishukuru serikali ya Poland kupitia Kituo cha Msaada wa Kimataifa cha Poland (PCPM) na Huduma za Afya Aga Khan Tanzania (AKHST) kwa hatua kubwa waliyopiga ya kutambua hitaji na kutoa ufadhili wa kiasi cha Dola za Marekani 760,000, sawa na Sh. bilioni 1.8," alisema.

Alisema lengo ni kuboresha huduma za dharura nchini katika kipindi cha miaka miwili na nusu iliyopita.

Dk. Manguna alisema njia ya kuboresha huduma za dharura Tanzania inaendelea na kupitia ushirikiano huo, watabadilisha mandhari ya huduma hizo nchini.

Alipongeza huduma za afya za Aga Khan Tanzania kwa kuwa ni mfano wa kuigwa katika ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi kwa juhudi zake za kusaidia serikali katika kuimarisha mifumo ya afya.

"Ingawa serikali imeanza kuchukua hatua za kutambua zaidi eneo hili na kuhakikisha kila kituo cha afya kina maarifa, ujuzi, miundombinu na vifaa vinavyohitajika kutoa huduma bora za dharura.

"Bado kuna upungufu wa rasilimali na ujuzi wa kutuwezesha kufanikisha kikamilifu. Kwa hivyo, Taasisi ya Huduma za Afya ya Aga Khan, kwa kushirikiana na Kituo cha Msaada wa Kimataifa cha Poland na serikali, kupitia mradi huu wamekuja na mpango wa kuboresha huduma za dharura na wameleta tofauti kubwa," alisema.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Poland, Jakub Wisniewski, alisema wanafurahi kushirikiana na Tanzania kupitia Taasisi ya Huduma za Afya ili kuimarisha huduma hizo za dharura.

Mtendaji Mkuu wa PCMC, Wojtek Wilk, alisema mradi huo uliogharimu Sh. bilioni 1.8, umewanufaisha zaidi ya watu 2,000 kupitia mafunzo mbalimbali.

Mratibu wa Mradi kutoka Taasisi ya Huduma za Afya ya Aga Khan Tanzania, Dk. Hussein Manji, alisema katika eneo la magonjwa ya dharura wamelenga kupunguza rufaa, vifo na kuwapa wananchi waliokuwa katika hali mbaya nafasi bora ya kupona.

# Wanafunzi wa kike wapatiwa mafunzo somo la TEHAMA

**Na Faustine Feliciane**

KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali za kuhimiza wasichana kusoma masomo ya Sayansi, taasisi ya Apps and Girls ya Dar es Salaam, imeendesha mafunzo kwa wanafunzi wa Sekondari kutoka shule tisa.

Mafunzo hayo ya vitendo yanalenga kuwainua wasichana katika kujifunza masomo ya sayansi na ubunifu wa vitu mbalimbali vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Carolyne Ekyarisiima, alisema wanashirikiana na shule mbalimbali kutoa mafunzo hayo ambayo yanamsaidia mwanafunzi kupata ujuzi wa kujiajiri.

Alisema moja ya sababu za kuanzisha mafunzo hayo ni kuondoa utofauti uliopo kati ya mwanafunzi wa kike na wa kiume katika kujifunza masuala ya kisayansi.

"Tunatoa mafunzo haya kuanzia ngazi ya shule za sekondari mpaka wale ambao hawapo kwenye mfumo rasmi wa elimu, tunawapa mafunzo ya teknolojia kama kutengeneza roboti, kupata ufahamu wa akili mnemba, lakini pia kuwapa mafunzo ya ujasiriamali," alisema.

Pia alisema wanafanya hivyo kuunga mkono juhudi za serikali kuhamasisha wasichana wengi kusoma masomo ya sayansi katika ngazi mbalimbali.

"Kila baada ya programu hii tunatoa nafasi kwa wanafunzi kushindana kuunda vitu mbalimbali vya tehama na kwa washindi waliofanya vizuri tunawapa zawadi kuwahamasisha wanafunzi mashuleni kusoma masomo ya sayansi," alisema.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Yas Tanzania, Rukia Mtingwa, alisema wameungana na taasisi hiyo kuisaidia serikali kuhamasisha wasichana kuchukua masomo ya sayansi kutokana na uchache wao kwenye masomo hayo.

"Tumeonelea kurudisha kwa jamii kile tunachokipata kutoka kwao kwa kusaidia vijana wetu kupata mafunzo haya ya Tehama ambayo yatawasaidia katika masomo yao na hata baada ya kumaliza masomo," alisema.

Mmoja wa wanafunzi hao, Maria Mtega, alisema mafunzo hayo yamewapa kujiamini katika kusoma masomo ya sayansi na kutambua namna ya kuanzisha mifumo mbalimbali ya teknolojia.

# Watoa maoni utambuzi, usajili wadau wa milki

**Na Munir Shemweta**

WADAU wa sekta ya milki mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, wametoa maoni mbalimbali kuhusiana na utambuzi na usajili wa wadau wa sekta ya milki nchini.

Mjadala kuhusu utambuzi na usajili wa wadau wa sekta ya milki ulifanyika jijini Dar es Salaama jana na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo Chama cha Wamiliki wa Ardhi na Nyumba Tanzania, Umoja wa Kampuni zinazomiliki na kuuza viwanja Dar es Salaama na Pwani, Chama cha Wapangaji na Wapangishaji na Umoja wa Wataalamu wa Milki tanzania (AREPTA).

Wakizungumza wakati wa kutoa maoni, walisema kuna haja kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kushirikiana na wadau ili kuifanya sekta ya milki kufanya kazi kwa ufanisi.

"Tunataka tuungane maana sisi si washindani. Tuungane katika kufanya kazi zetu," alisema Emilian Rwejuma, Mwenyekiti wa Umoja wa Kampuni Zinazomiliki na Kuuza Viwanja Dar es Salaam na Pwani.

Mwenyekiti wa Chama cha Wapangaji na Wapangishaji, Abdallah Msangama, amesema maisha yamekuwa hatarishi kutokana na migogoro mbalimbali kama vile ya upangaji inayojitokeza huku akisisitiza makazi bora ni yale yasiyo na migogoro.

Pia aligusia suala la utoaji elimu kwa wapangaji na kusema serikali kwa sasa inakosa fedha nyingi kupitia masuala ya kodi na kusisitiza utoaji elimu kwa wenye nyumba na wapangaji ili kuelimika na kuepuka changamoto ndogo ndogo alizozieleza kuwa hazina maana.

"Niishukuru Wizara ya Ardhi kwa kuleta maono ya mjadala wa sekta ya milki ya namna tunavyokwenda katika kuiboresha sekta hii," alisema.

Rais wa Wataalamu wa Milki Tanzania (AREPTA), Andrew Kato, alisema, kumekuwa na changamoto kadhaa katika tasnia ya milki jambo linaloifanya sekta hiyo kutoheshimika na kutaka sasa iheshimike kama ilivyo kwenye nchi zingine.

Alisema ni vizuri pakawapo utaratibu mzuri wa upangishaji nyumba tofauti na ilivyo sasa ambapo hakuna utaratibu maalum jambo alilosema linasababisha madalali kuchukua fedha kutoka kwa wapangaji, wanunuzi, wauzaji na wenye nyumba

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Milki katika Wizara ya Ardhi, Nyunba na Maendeleo ya Makazi, Wilson Wairara, alisema wizara haihitaji kumtenga mtu yeyote katika suala la milki bali kuweka utaratibu mzuri unaoweza kuchochea weledi na ufanisi katika kufanya shughuli zake.

Kuhusu maono na malengo ya wizara katika kukuza sekta ya milki, alisema kwa sasa suala la kanzidata kwa wadau wa milki linatiliwa mkazo kwa kuwa kama idadi ya wadau haijulikani itakuwa ni changamoto hata kufanya mipango madhubuti ya kuisukuma sekta ya milki.

"Tunakwenda kuleta mfumo mzuri utakaoweza kusaidia katika kukusanya taarifa mbalimbali zikiwamo za makampuni kitu ambacho ni muhimu sana," alisema.

Aliongeza kuwa wizara haitafanya kazi zake bila ushirika mkubwa wa wadau wa sekta ya milki, hivyo msisitizo wake ni kushirikiana na wadau katika kuiboresha au kurahisisha utekelezaji wa shughuli za sekta milki.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia Kitengo cha Milki, inaendesha mijadala ya pamoja na wadau kwa lengo la kupata maoni kuhusu utambuzi na usajili wa wadau wa sekta ya milki ili kuboresha na kukuza sekta ya milki nchini.




Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Sultan Ng'aladzi (kushoto) na mfanyakazi wa taasisi hiyo Rachel Lucumay (kulia) wakikabidhi msaada wa mafuta, vyakula na sabuni kwa msimamizi wa kituo cha watoto yatima na wenye uhitaji maalum cha Light In Africa, Mariam Mkali cha mji mdogo wa Mirerani, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# CTI yaipongeza serikali kuendelea kuwa sikivu

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), limepongeza serikali kwa kuendelea kuwa sikivu na kutatua changamoto nyingi za wenye viwanda zikiwamo za kikodi zilizokuwa sumbufu.

Mkurugenzi Mtendaji wa CTI, Leodegar Tenga, alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa shirikisho hilo.

"CTI itaendelea kufanya kazi kwa karibu na serikali kufanikisha maendeleo ya viwanda ili kukuza uchumi na kwenda sawa na azma ya serikali ya awamu ya sita ya kujenga uchumi wa viwanda," alisema.

Kuhusu changamoto za wenye viwanda, Tenga alisema ni zile zile na serikali imefanya jitihada kubwa kuzitatua kama kodi zisizokandamiza viwanda, sheria na tozo ambazo zilikuwa zinakwamisha viwanda.

"Sisi na serikali tunaendelea vizuri sana na masuala haya si mepesi kwa sababu inachukua muda sana kujadiliana na kufikia muafaka, lakini kwa dhati kabisa naishukuru serikali kwasababu imekuwa ikitusikiliza kila tunapowasilisha changamoto zetu," alisema.

Tenga alisema wamefanya mkutano mkuu ulioenda sambamba na mjadala kuhusu umuhimu wa kuzingatia masuala ya mazingira na kijamii na uwajibikaji na wanachama wa shirikisho hilo walishiriki kujadili na kutoa mapendekezo yao. "Nimefurahi sana kuona mjadala ulikuwa mzuri nawashukuru wanachama kwa kuja kwa wingi na tumewasisitiza wenye viwanda kwamba ni muhimu kuzingatia masuala ya mazingira kwani ni ajenda ya dunia kutunza mazingira," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Viwanda, Fatma Khamis, alipongeza CTI kwa kufikisha miaka 31 tangu kuanzishwa kwake, huku ikiendelea kuwa imara na kuwa na sauti kubwa kwa wenye viwanda.

Alisema wenye viwanda wanatakiwa kuzalisha bidhaa kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira, mila na desturi za watanzania na kuhakikisha wazawa wananufaika na uwekezaji wao hapa nchini.

"Hivi sasa ajenda ya mazingira ni ya dunia nzima kwa hiyo nawashauri kila mnachofanya muangalie kama mazingira yetu yanakuwa salama kwasababu bila kutunza mazingira tutaangamiza kizazi kijacho," alisema.

"Nawapongeza CTI kwa kuendelea kuwa imara kwa miaka 31 ya uhai wake, siyo rahisi kwa taasisi kama hizi kuwa imara kwa miaka mingi kiasi hicho kwasababu tunashuhudia nyingi zinakufa kwa changamoto mbalimbali kama ukosefu wa fedha na migogoro lakini hawa wasimama imara mpaka sasa," alisema.

Fatma alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na ya Muungano zitaendelea kuimarisha mazingira ya kufanya biashara, ili kuvutia uwekezaji wa ndani ya nchi na wale wanaotoka nje ya nchi. Alisema mfano wa dhamira hiyo ni kamati iliyoundwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan kwaajili ya kuangalia mfumo wa kodi na kutoa mapendekezo ya namna ya kuboresha.

"Kupitia 'blue print' tumeangalia changamoto mbalimbali za biashara kama mlolongo wa leseni ambazo mwekezaji anatakiwa kuwa nazo kabla ya kuanza uwekezaji, kwa hiyo kuna changamoto nyingi zimeshafanyiwa tathmini," alisema Fatma. "Mmeona hata namna Rais Samia anavyosafiri mataifa mbalimbali duniani kutafuta wawekezaji na safari zimeshaanza kulipa kwasababu wote ni mashuhuda wa namna wawekezaji kutoka nje ya nchi wanavyozidi kumiminika hapa nchini," alisema.



## Wanafunzi 500 kaya maskini kupatiwa sare, madaftari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri amezindua kampeni ya kuwawezesha kusoma wanafunzi zaidi ya 500 wilayani hapa wenye mahitaji maalum kutoka kaya maskini.

Kampeni hiyo ya nipendezeshe nisome inaratibiwa na kituo cha redio cha C FM cha jijini hapa

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Shekimweri alisema pamoja na serikali kuwekeza kwenye sekta ya elimu, baadhi ya watoto kwenye kaya maskini nchini, wanashindwa kwenda shule kwa sababu mbalimbali.

Aliitaka jamii kujenga utamaduni wa kusaidia watoto hao wenye uhitaji ili waweze kupata haki yao ya msingi ya elimu.

"Serikali yetu imefanya uwekezaji katika sekta ya elimu nchini kwenye miundombinu ya kujifunzia na kufundishia, pia imeboresha maslahi ya watumishi na kutoa elimu bila malipo," alisema.

Hata hivyo, alisema kuna changamoto kwa baadhi ya watoto kushindwa kwenda shule kutokana na baadhi yao kufiwa na wazazi.

Shekimweri, alisema ni matumani yake kampeni hiyo itasaidia wanafunzi wengi kutoka familia maskini kupata vifaa vya shule, sare, madaftari na mahitaji mengine muhimu kwa ajili ya shule.

Mwalimu Mkuu wa Shule Msingi Dodoma Makulu, Amon Sebyiga, alisema wanafunzi 30 wa shule hiyo watanufaika na mpango huo.

"Tumeanza na wanafunzi hawa wa madarasa ya chini kama wasipopata mahitaji ya muhimu wanaweza kuacha shule," alisema

Sebyiga, alisema katika awamu hiyo wamechukua wanafunzi 30 kuanzia darasa la kwanza hadi la tatu kila moja 10 kwa uwiano wa wasichana watano na wavulana idadi kama hiyo.

Mwenyekiti wa kampeni hiyo kutoka C FM, Sonatah Nduka, alisema wanafunzi hao wenye mahitaji maalum wanalenga kuwapatia sare, madaftari, chakula na mahitaji mengine muhimu.

"Kupitia kampeni hii tunalenga kuwafikia watoto wenye uhitaji katika mwaka wa masomo 2024/25 zaidi ya 500 kwa kuwapatia vifaa ili waweze kusoma kama ilivyo kwa wengine," alisema.

# UDOM yazindua mafunzo ufuatiliaji miradi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHUO Kikuu cha Dodoma (UDOM) kimezindua mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo ili kuisaidia serikali kukamilisha kwa wakati.

Akizungumza jana jijini hapa baada ya kufungua mafunzo hayo kwa wataalamu wa sekta mbalimbali nchini, Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Lughano Kusiluka, alisema ni muhimu kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa wakati.

"Eneo la ufuatiliaji na tathmini ya miradi ni nyeti na muhimu kuanzia hatua ya kuanza kubuni hadi utekelezaji wake, ikiwamo ya ujenzi wa miundombinu au utafiti," alisema Kusiluka.

Alionya kuwa bila kuweka utaratibu mzuri wa usimamizi na tathmini, mradi hautatekelezeka na kuliingizia hasara Taifa.

Alisema sababu hiyo ni chanzo cha miradi mingi kushindwa kukamilika kwa wakati.

Kusiluka, alitoa wito kwa wasimamizi wa miradi kujiunga na mafunzo hayo ili kukabiliana na vikwazo vya ufuatiliaji.

> **"Watoto wasio na 'uniform' (sare) wasifukuzwe darasani. Tunachotaka watoto wapate elimu na katika mkoa wa Singida kwa sasa tuna operesheni ya kutokomeza matokeo ya daraja...**

"Mojawapo ya eneo linalofundishwa hapa ni kuangalia mradi wa aina gani ulikuwa unahitaji kutekelezwa kwa kiasi gani na mambo yanatakiwa kufanyika lini na wapi ili wasimamizi waweze kuwa na matokeo yanayotarajiwa,"alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Maendeleo wa Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), Dk. Ajali Mustafa, alisema matarajio yao kupitia mafunzo hayo ni kutengeneza wasimamizi bora na watakaoongoza miradi ya serikali.

Dk. Mustafa, alisema lengo la mafunzo hayo ni kupeleka maarifa kwa watumishi wa taasisi za umma na binafsi nchini.

"Msukumo wa kuanzisha kozi hii ni kutokana na uhitaji mkubwa wa wataalamu wenye ujuzi wa usimamizi wa miradi na kwa kuwa UDOM ina wataalamu wabobevu kwenye sekta hii, imekuwa vema kuanzisha kozi fupi ili kuwafikia walengwa,"alisema.

Awali Ofisa Usimamizi wa Milki kutoka Shirika la Nyumba Zanzibar, Juma Hassan, alisema mafunzo hayo yatasaidia miradi kukamilika kwa wakati.



Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Kitengo cha Milki Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Wilson Wairara akizungumza wakati wa mjadala kuhusu utambuzi na usajili wa wadau wa sekta ya milki uliofanyika jijini Dar es Salaama jana. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# CCM yawaonya watendaji goigoi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) wilayani hapa Mkoa wa Singida kimewaonya watumishi wa serikali wanaokiuka maadili ya kazi na kusababisha wananchi kukichukia.

Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Manyoni, Jumanne Makhanda, alitoa onyo hilo kwenye kikao cha Baraza la Jumuiya ya Wazazi ya chama hicho ya wilaya hiyo juzi mjini hapa.

Makhanda, alifafanua kuwa ametoa onyo hilo baada ya kubaini kuwa kuna watumishi wa serikali hawatimizi majukumu yao ipasavyo hali inayosababisha wananchi kuichukia CCM.

Alisema chama hicho hakitakubali kuona wananchi wanakichukia kutokana na watendaji hao na kusababisha kukosa imani nacho.

Kwa upande mwingine, Makhanda alimpongeza Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha katika wilaya hiyo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Vilevile, aliwapongeza wakuu wa idara katika Halmashauri ya Wilaya hiyo na Halmashauri ya Mji wa Itigi kwa kufanya kazi kwa weledi na kutaka mfano wao uigwe na watu wao wa chini ili kuleta maendeleo ya haraka kwa wananchi.

"Nawaomba wajumbe wa Baraza la Wazazi Wilaya kutimiza wajibu wenu kwenye maeneo yenu lakini pia kwa Wakuu wa Idara fanyeni kazi kwa bidii na weledi zaidi kwa maslahi ya wananchi," alisema.

Kuhusu mikopo, aliwataka maofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri kuharakisha mchakato wa kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa wananchi ili waanzishe miradi ya ujasiriamali.

Aliwashukuru wananchi kwa kuiunga mkono CCM katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika Novemba 27, mwaka huu na kuibuka na ushindi mnono.





# Viongozi wa siasa Afrika, Ulaya wajadili demokrasia dunianiu

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya viongozi wa siasa wa nchi za Ulaya na Afrika wapo visiwani Zanzibar kujadili kukuza demokrasia duniani.

Akifungua mkutano wa saba wa Umoja wa Vyama vya Siasa Afrika (APCA) unaohudhuriwa na viongozi hao wakiwamo wa nchini, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haruon Ali Suleiman, alisema katika nchi ni muhimu kujadili kudumisha amani, utulivu na utawala bora kwa maslahi ya wananchi na maendeleo.“Sisi Zanzibar na Tanzania tumefanikiwa kuwa na utawala bora, amani na utulivu na ndio maana tumeweza kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK),” alisema Haruon.

**“Mnada huu utaendeshwa kwa usalama mkubwa kwa kuwa madini hayo hususan Tanzanite yana thamani kubwa. Serikali imeimarisha ulinzi ili kujihadhari na watu wasio waaminifu,” alisema.**

Alitaja baadhi ya mambo yatakayojaliwa katika mkutano huo kuwa ni hali za nchi na mabadiliko ya kisiasa barani humo katika chaguzi zijazo na kubadilishana uzoefu utawala bora na uwajibikaji.

Mwenyekiti wa APCA kutoka Nairobi nchini Kenya, Duncan Kupngeno, alitaja mambo mengine yatakayojadiliwa kuwa ni kusaidiana katika siasa kwa kila nchi kuelezea uzoefu wake.

Kupngeno, alisema pia watajadili jinsi ya kuwasaidia viongozi wa Afrika kuhakikisha wanafuata demokrasia kuhudumia wananchi.

Mkutano huo ulitoa fursa kwa viongozi wa siasa wa Marekani na Uingereza kujadili mfumo wa vyama vyao na kutembelea maeneo ya kihistoria visiwani hapa.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba,Sheria,Utumishi na Utawala bora Haruon Ali Suleiman akizungumza wakati akifungua mkutano wa saba wa umoja wa vyama vya siasa barani Afrika (APCA) uliofanyika juzi visiwani Zanzibar. **PICHA: MAELEZO ZANZIBAR**

## Watakiwa kushirikisha jamii kudhibiti uvuvi haramu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMENEJA wa hifadhi za bahari na wakuu wa doria wametakiwa kushirikiana na jamii kudhibiti uvuvi haramu visiwani hapa.

Wito huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa Idara ya Uhifadhi wa Bahari, Dk. Makame Omar Makame wakati wa kikao cha tathmini ya doria ya Novemba mwaka huu kilichofanyika visiwani hapa.

Dk. Makame, alisema licha ya kuwepo kwa vitendo vya uvuvi haramu, kiasi kikubwa bahari imerudi katika hali yake ya ubora kutokana na kudhibiti zana haramu za uvuvi katika maeneo ya hifadhi za bahari.

Alisema hatua zaidi zitaendelea kuchukuliwa kwa wavuvi watakaoendelea kuvua samaki na mazao ya bahari ndani ya mwamba na nyavu za utari na madema ya waya.

Alisema uvuvi haramu unachangia uharibifu wa mazingira na mazalia ya samaki, hivyo ni vyema kila mmoja kuwajibika kudhibiti uvuvi huo.

Nuru Said kutoka Taasisi ya Mwambao, alisema wataendelea kushirikiana na Serikali kuimarisha uhifadhi wa bahari, rasilimali na mazingira.

Nuru, alisema bahari ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya taifa, hivyo ni vyema itunzwe na kuhifadhiwa ili kukabiliana na uharibifu na uchafuzi wa bahari.

Ofisa Uvuvi wa Wilaya ya Kati Unguja, Ali Mwalim Mahafoudh, alisema elimu zaidi ya umuhimu wa matumizi mazuri ya bahari na ukataji wa leseni kwa wavuvi na vyombo vyao itaendelea kutolewa kwamujibu wa sheria.

# SMZ kufumua mpango wa sera mpya ya ujenzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ina mpango wa kuanzisha sera mpya ya ujenzi ili kuendana na mabadiliko yanayoendelea kutokea duniani katika sekta ya ujenzi.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), Yussuf Majid Nassor wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa wadau na watoa huduma katika sekta ya ujenzi.

Nassor, alisema hatua hiyo inakuja baada ya kubaini kuna changamoto katika sera hiyo ya ujenzi visiwani hapa licha ya kuwepo makandarasi na wakadiriaji wa majengo waliobobea.

Alisema serikali hiyo ina mpango wa kuanzisha sera hiyo kuendana na wakati wa sasa na muhimili mkubwa kwa maendeleo ya miradi ya ujenzi visiwani hapa.

Awali akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabari, alisema vifaa bora vya ujenzi ni msingi wa ufanisi wa miradi ya maendeleo.

Shabari, alisema ufanisi huo unaanzia kwenye majengo ya kawaida, umma na miundombinu mikubwa ya barabara, madaraja na majengo ya umma.

Alisema ufanisi wa miradi hiyo unategemea ubora wa vifaa vya ujenzi, hivyo ni muhimu kwa wakadarasi kuhakikisha umethibitishwa na ZBS.

Alisema Serikali hiyo itahakikisha mazingira ya biashara katika sekta ya ujenzi yanakuwa rafiki na salama ili kuendelea kutoa bidhaa bora na kutekeleza miradi kwa ufanisi na vigezo vinavyokubalika.

“Natoa wito kwa wadau wote wa vifaa vya ujenzi, wazalishaji na wasambazaji kujitokeza kwa wingi kupima bidhaa zao kwa viwango vinavyokubalika na ZBS, “ alisema.

Aliwataka wadau hao kupeleka bidhaa zao katika vituo vya ZBS kupima na kuthibitisha ubora wake kabla ya kuuzwa na kutumika katika miradi ya ujenzi.

Alisema Serikali itahakikisha gharama za kupima vifaa vya ujenzi zinakuwa rahisi na kufikiwa na wadau wote.

Alisema hatua hiyo itawawezesha wafanyabiashara wa vifaa vya ujenzi kufuata taratibu, kuongeza usalama na ufanisi wa miradi. “Nachukua nafasi hii kukuhimizeni kuwa waadilifu katika kuhakikisha ubora wa bidhaa zenu unafata viwango vilivyowekwa ili kwenda na matakwa ya viwango kitaifa na kimataifa na kupata majengo bora na salama, “alisema

Hata hivyo, alisema ubora wa vifaa vya ujenzi una mchango mkubwa kulinda maisha ya wananchi , kuimarisha uchumi na kupunguza gharama zinazoweza kutokea kutokana na uharibifu wa majengo na miundombinu.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Ujenzi na Uchukuzi, Makame Haji Machano, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wadau hao kutumia vifaa bora vya ujenzi na kuwepo kwa mabaraza ya uchunguzi wa vifaa Zanzibar.

Alisema wafanyabiashara wa vifaa vya ujenzi walikuwa wakipeleka Tanzania Bara sampuli za vifaa kupima katika maabara, lakini kwa sasa ipo Zanzibar .



**P FUNKY**

UKURASA 12

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI DESEMBA 14, 2024



# KAACHWA MPWEKE, Diamond yulee Ulaya

SAKATA la wanamuziki Diamond Platnumz na Willy Paul kutoka Kenya, linazidi kufuka moshi na kusababisha kuwepo na mpasuko wa maoni kuhusu ugomvi huo.

Hata hivyo, idadi kubwa ya wasanii na wachambuzi wa burudani wanamtetea Diamond kutokana na hatua yake ya kuondoka eneo la tukio haraka wakati Willy Paul alipoanzisha vurugu akishinikiza kuwa wa mwisho kupanda jukwaani.

Hivi karibuni Diamond na timu yake akiwamo Zuchu walikuwa nchini Kenya kwa ajili ya kutoa burudani katika tamasha moja, hata hivyo hakupanda jukwaani baada ya kutokea vurugu na kuvurugika kwa ratiba.

Willy Paul, ambaye amebeba dhana ya Wakenya kwanza, amezidi kukosolewa na wadau mbalimbali akielezwa ni mtu anayetukuza ubaguzi, chuki na fitina. Vyombo vya habari mbalimbali pamoja na wasanii kutoka nchini humo wameungana kupinga kitendo hicho ambacho kinaweza kugawanya raia wa nchi hizo mbili ambazo zinategemeana kwa kila sekta.

Baada ya tukio hilo ambalo watu wengi wanaamini limempatia umaarufu Willy Paul, angefanya kazi nzuri ambayo ingeshtua tasnia ya muziki, badala yake amekuwa akionekana na Mchekeshaji Eric Omondi, wakinadi shoo yao.

Wanaeleza kubaki na Omondi ni kosa kubwa amefanya, kwani Diamond ambaye anapigana naye na anamuona kama adui, yeye anaendelea kuchapa kazi akiwa nchini Ufaransa.

"Anachokifanya Willy Paul hakina maana katika sekta ya burudani, anataka kusababisha mgawanyiko ambao hauna tija kwa sababu Tanzania kuna Wakenya wengi wanafanya kazi, sisi ni ndugu lazima tuwe na upendo," amesema mtangazaji wa Kenya KG Chipande, katika kipindi chake kimoja.

Chipade amesema hakuna mtu mwenye akili anayeweza kuunga mkono kile alichofanya mwanamuziki huyo na kueleza amekosa weledi na uanataaluma wa kisanii kufikisha ujumbe wake.

BASI SAWA

## Shamsa Ford, mumewe hawataki kiki



MSANII wa filamu za Bongo Muvi, Shamsa Ford, amesema yeye na mume wake Mlilo, ni watu wasiopenda kiki ambazo zinawaondolea heshima na maadili.

Amesema kuwa anamshukuru Mungu kwa kumpata mume ambaye anamuunga mkono na tena msanii, hivyo hakuna umuhimu wa kutafuta umaarufu mwingine kwa kufanya matukio yanayoweza kuwachafua.

"Mimi na mume wangu Mlilo tunaishi katika maadili na kuheshimiana, hatuna haja ya kutafuta kiki kwa kufanya vitu ambavyo vinaweza kutuondolea utu, tunachoamini Mungu ametupendelea kuwa pamoja," amesema Shamsa.

## Baba Levo amkimbia Diamond



MWANAMUZIKI na mtanagazaji, Baba Levo, amesema hataki kufanya kazi ya muziki na bosi wake Diamond Platnumz, kwa sababu atamrudisha nyuma kimaendeleo.

Amesema hivi karibuni Diamond alimtumia sauti ya wimbo ili kufanya kolabo nyingine, lakini anamkimbia kutokana na mahitaji ya kurekodi video inakuwa kubwa kiasi ambacho hataweza kumudu.

"Kazi ya muziki namwanchi Diamond mwenyewe, hapa nilipo namkimbia ili nisifanye kazi naye kwani jamaa anataka video ya gharama kubwa na mimi kwa sasa sina pesa, najenga nyumba yangu sitaki kufilisika," amesema Baba Levo.



## P FUNKY ASISITIZA KUTAMBULIWA

MTAYARISHAJI mkongwe wa muziki, P Funky, amesema mfumo wa muziki umeshindwa kuwatambua watu muhimu katika nyimbo.

Amesema changamoto inayoikabili tasnia ya muziki ni kuwaacha pembeni watayarishaji wa muziki na watunzi wa mashairi, badala yake inamtambua mwimbaji pekee.

"Ni muhimu kuweka mfumo ambao unawatambua mwimbaji, mtayarishaji na mtunzi wa mashairi ili kila mtu anufaike kwa ubunifu wake," amesema P Funk.



## Chino msimuulize kuhusu Sumu

MKALI wa muziki wa Amapiano, Chino Kidd, amesema jina la 'Sumu' ambalo ameipa EP yake mpya yenye nyimbo sita haina maana na tuhumu aliyopatiwa siku za nyuma.

Chino, amesema EP yake hiyo ambayo itazinduliwa Ifakara mkoani Morogoro ambako alikulia, itahudhuriwa na mastaa kibao akiwemo Marioo ambaye huko nyuma hawakuwa na maelewano mazuri kiasi cha kushtumiana kuwekeana sumu.

Amesema kwa sasa wanamuziki hao wako vizuri na ndio maana wote watakuwepo katika tukio hilo, hivyo akawataka mashabiki zake wasiweke maana tofauti kuhusu jina hilo.

## DUNIA SI MBAYA, WALIMWENGU WABAYA

**Na Adam Fungamwango**

UKISIKILIZA hadithi nyingi na mambo mengi ya zamani na hata ukisoma kwenye vitabu mbalimbali vyenye kuheshimika, utagundua hakuna kitu kipya hapa duniani kinachofanyika.

Yote ni yale yale tu. Ni kama vile wanasayansi wanavyosema dunia inajizungusha yenyewe kwenye mhimili wake na kweli yote yanayofanyika yanajirudia tu.

Tena kuna vitu vingine vilifanyika zamani hadi leo hii havijafanyika tena. Vinavyoendelea kujirudia ni baadhi ya mambo machache tu yaliyofanyika miaka milioni nyingi huko nyuma.

Ndiyo maana utasikia watu wanakwambia maisha ya sasa ni magumu. Lakini ukisikia nyimbo za miaka 50 nyuma, utakuta wanaimba maisha ya sasa ni magumu. Ina maana yalianza kuwa magumu tangu zamani. Hivi sasa kuna udanganyifu wa mapenzi. Ukisoma vitabu vya miaka mingi nyuma, utakuta pia kulikuwa na udanganyifu.

Leo ni mada hii tutaziangalia nyimbo ambazo zinazongumzia dunia, raha, matatizo yake na vituko zilizotungwa miaka ya 1980 mwanzoni hadi mwishoni.

### Dunia Duara-Shaaban Dede

Shaaban Dede akiwa na Bima Lee, alitunga kibao cha 'Dunia Duara'. Hiki kinazungumzia juu ya mtu anayechekwa na wenzake kuwa hana kitu.

Lakini mwenyewe anajipa matumaini kuwa dunia ni duara na huzunguka, hivyo anajua kesho atapata kwa jinsi anavyojituma. Anasema jua halina mpaka, huangaza pote kwa hiyo ipo siku na yeye ataangaziwa, kwani kama samaki baharini, wadudu mapangoni na wanyama porini wanaishi, basi kwa kudra za Mungu na yeye atapata tu.

### Dunia Uwanja wa Fujo-Marijani

Jabali la Muziki Marijani Rajab, yeye akatunga kibao cha 'Dunia Uwanja wa Fujo'. Anawatahadharisha wote wanaojimwambafai na kuiona dunia kama yao, kuwa walikuwepo watema, wafalme wenye nguvu, lakini leo hii hawapo.

Alikuwepo Firauni, Hitler, Nduli Idd Amini ambao historia ni inasema ni moja kati ya viongozi wababe kuwahi kutokea duniani, lakini kwenye dunia hii hakuna mbabe kushinda Mwenyezi Mungu.

Kwa maana hiyo anawaasa watu hususan wanaopewa dhamana, kuishi vizuri na watu, kwa sababu ubabe hauna maana akamalizika kwa kusema kwenye dunia hii 'kula ugali wako ukalale'.

### Dunia-Remmy Ongalla

Remmy Ongalla kwenye fasihi yake ya wimbo huu wa 'Dunia' anasema yote ambayo binadamu atakayofanya hapa duniani, ikiwa ubaya au wema, atalipwa hapa hapa ulimwenguni.

Anasema kwa Mungu hatupajui, hivyo binadamu anatakiwa kutenda wema, kwani kuna baadhi ya watu hudhulumu wengine kwa vyeo vyao, wadhifa, pesa na umaarufu.

### Dunia-TX Moshi William

Akiwa na bendi ya Polisi Jazz, kabla ya kujiunga bendi ya Juwata Jazz, alitunga kibao kisemacho 'Dunia'. Anauliza, mwezi na nyota usiku zinang'aa bili yake analipa nani? Na ilitakiwa kabisa aulizwe anayelipwa bili ni nani? Huyo ni mwenyezi Mungu. Yeye kila kitu hutoa bure kwa waja wake.

### Dunia Imani Imekwisha-Marijani

Hapa Marijani amerudi tena hapa na wimbo wa 'Dunia Imani Imekwisha'. Yoyote aliyedhani eti sasa ndiyo kuna dhana hiyo, lakini hata miaka ya 1970 hadi 1980, kulikuwa na matendo kiasi cha kuonekana dunia imani yake ni ndogo. Watu wanaibiana. Wanatapeliana. Wanadhulimiana. Kuna wanaodhulumu watoto yatima. Wanaotaka kuwaua wazazi wao ili warithi mali na mengine mengi.

FILAMU

# Kijumbe, laki si pesa



**Na Adam Fungamwango**

UTAMU wa filamu hii, pamoja na mafunzo kwenye jamii, lakini ni kumuangalia Riyama Ally, akipambana na Bi Hindu kwenye vita ya maneno. Wote watu wenye maneno ya karaha na shombo. Ni watu wa vijembe. Hapa sasa wamekutana.

Filamu hii ya 'Kijumbe' ina ujumbe kuwa unaweza kufanya kitu ukadhani unamkomoa uliyemfanyia, kumbe athari zikarudi pia upande wako.

Kazembe, baada ya kujua kuwa dada yake Riyama anacheza upatu na kesho ni zamu yake ya kuchukua pesa, anakwenda kwa kijumbe ambaye ni Bi Hindi kumlaghai kuwa ametumwa na dada yake amemchukulia pesa zake.

Bi.Hindu bila ya kujua hili wale lile, anamkabidhi Kazembe pesa kiasi cha shilingi laki moja unusu. Kumbe sivyo alivyodhani. Kazembe anakwenda kutangaza ufalme kwenye baa. Riyama anatimba kwa kijumbe kudai pesa zake. Bi Hindu anamwambia alimpa kaka yake Kazembe. Hapo ndipo timbwili linapoanza. Kila mmoja anampachika mwenzake mineno ya shombo.

Riyama anakwenda kwa kaka yake kumuuliza. Kazembe anakataa. Mume wa Riyama naye anataka pesa zake alizompa mkewe kwa ajili ya mchezo, kwa sababu aliambiwa kesho anakwenda kulipwa.

Pesa hazijapatikana, mume anatishia kumpa talaka mkewe. Zawadi, mpenzi wa Kazembe baada ya kupata taarifa nyingi kuhusu jambo hilo, anaamua kumsaidia kwa kuiba pesa shilingi laki moja unusu nyumbani kwao ili deni lilipwe.

Anampa mpenzi wake Kazembe akalipe, lakini kijana huyo anakwenda kuzitumia vibaya, kama alivyofanya zile za kwanza.

Bi Hindu anamshutumu Kazembe. Riyama anamdai Bi Hindu. Mume wa Riyama naye anaamua kumpa talaka moja mkewe kwa kutoona pesa za mchezo, Zawadi naye anampiga kibuti Kazembe kwa kosa la kutopeleka pesa ili deni lilipwe.

Hili linamfanya Kazembe kukosa raha kwani alilolifanya limemrudia yeye na dada yake Riyama ambaye ameachwa na mumewe. Anaamua kuomba radhi. Anatafuta pesa. Anazipata laki na nusu na kumrudishia Bi. Hindu. Naye anamlipa Riyama. Anarudiana na mumewe. Kazembe anatafuta laki unusu zingine na kumpa Zawadi ili azirudishe kwao, na hapo uhusiano wao ukarejea.

# Tiwa Savage sio tapeli

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Tiwa Savage ametoa siri kuhusu uhusiano wake wa kimapenzi, akisema hajawahi kumuacha mwanaume baada ya kumlaghai.

Mwimbaji huyo alifichua hivi karibuni kuwa alisisitiza kuwa licha ya kuwa na upendo, lakini kudanganya sio kikwazo kwake katika mahusiano.

"Nilishawahi kutapeliwa. Niligundua hilo na kusamehe kila wakati. Kila mwanaume niliyewahi kuwa naye si kweli kuwa nilimdanganya, na sijawahi kuwaacha kwa sababu hiyo. Nimeondoka kwa sababu nyingine, lakini si kwa sababu walidanganya. Kudanganya sio shida yangu." Amesema.






## Phyna hataki jina la familia

ALIYEKUWA mshindi wa Big Brother Naija, Phyna ameeleza kuwa kuacha jina la ukoo la familia yake la Otabor, inatokana na kuumizwa na kudharauliwa.

Akizungumza na TVC News, amesema kwa muda mrefu amekuwa akiishi na hisia kali baada ya kutengwa na kudhulumiwa na familia yake.

"Hili linatokana na mimi kukubali jinsi wamekuwa wakinichukulia kwani hawajawahi kunichukulia kama mtu wao. Niliamua kuondoka kwa sababu nilichoka kumomba mtu yeyote kuwa katika maisha yangu," amesema Phyna.


## Megan Fox ana wakati mgumu

MWIGIZAJI wa Marekani, Megan Fox, ameripotiwa kuwa na wakati mgumu baada ya kutengana na mpenzi wake Machine Gun Kelly (MGK) mwezi mmoja baada ya kutangaza ni mjamzito.

Kulingana na jarida la People, linasema kwamba amekuwa na kipindi kigumu kuwepo kwa mgawanyiko huo, huku chanzo kimoja kikisema msanii huyo amekuwa kama amefadhaika.

Chanzo kingine kililiambia jarida hilo kuwa Megan na Machine huenda wakarudiana licha ya kuwa na tofauti zao.





## Selena apata wake

MWANAMUZIKI na msanii wa filamu kutoka Marekani, Selena Gomez, ametangaza uchumba wake na mtayarishaji wa muziki Benny Blanco, ambaye wamekuwa na uhusiano kwa mwaka mmoja.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, amechapisha picha akiwa amevaa pete yake ya uchumba na kuandika ujumbe kuwa milele inaanza sasa.

Blanco alionyesha furaha yake kwa kuandika maoni yake "Hei subiri... wewe ni mke wangu," na watu wengine mashuhuri walimpongeza kwa hatua yao hiyo.

## Jamie Foxx asimulia ugonjwa wake

BAADA ya kulazwa hospitalini kwa kuugua ghafla mwaka uliopita, mwigizaji wa Marekani Jamie Foxx amefichua kwamba alikuwa na tatizo la damu kwenye ubongo na kumsababishia kiharusi.

Kupitia mtandao wa Netflix, Foxx, amesema tatizo hilo lilianza kwa kupata maumivu makali ya kichwa na aliomba dawa aina ya asprini.

"Nilikuwa nikiumwa sana na kichwa na nikamwomba kijana wangu anipe aspirini. Na nikagundua haraka kwamba unapokuwa katika dharura ya matibabu, vijana wako hawajui una tatizo gani ni tatizo. Kabla sijapata aspirini nilianguka na sikumbuki siku 20" amesema Foxx.





# Serikali yarejesha mnada madini ya vito Mirerani

**Na Mwandishi Wetu,** SIMANJIRO

SERIKALI imeurejesha rasmi, mnada wa ndani wa madini ya vito katika Mji wa 'Tanzanite' ulioko Mirerani Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara baada ya taratibu za marekebisho ya kisheria kukamilika juu ya uendeshaji wa mnada huo uliosimama kwa muda.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, anatarajiwa kuzindua mnada huo leo (Desemba 14), ambao licha ya kuongezea thamani madini hayo, una nia ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara ya madini ya vito na usonara Barani Afrika.

Kurejea kwa mnada huo ni utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa ufunguzi wa kiwanda cha kusafisha dhahabu jijini Mwanza, Juni 13, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Waziri Mavunde, madini hayo ya vito yanauzwa kwa mnada kama mkakati wa serikali, kupitia Wizara yake kuyatangaza na kuyaongezea thamani kimataifa.

Alisema hatua ya kuzindua mnada huo ni jitihada nyingine za serikali kudhibiti utoroshwaji wa madini hayo kwenda nje ya nchi, unaofanywa na watu wasiokuwa waamifu.

Aidha, mnada huo unalenga kuwasaidia wachimbaji wa ndani kuuza kwa bei ya ushindani inayoendana na soko la dunia na kukuza uchumi wao.

**"Mnada huu utaendeshwa kwa usalama mkubwa kwa kuwa madini hayo hususan Tanzanite yana thamani kubwa. Serikali imeimarisha ulinzi ili kujihadhari na watu wasio waaminifu," alisema.**

Mavunde, alisema mnada huo ambao unafanyika kwa mara ya kwanza akiwa waziri wa wizara hiyo, utashirikisha wanunuzi kutoka ndani na nje ya nchi, na kwamba atakayenunua madini hayo ni yule atakayeshinda bei iliyowekwa.

"Mnada huu utaendeshwa kwa usalama mkubwa kwa kuwa madini hayo hususan Tanzanite yana thamani kubwa. Serikali imeimarisha ulinzi ili kujihadhari na watu wasio waaminifu," alisema.

Mavunde, alisema mnada huo utaiwezesha serikali kupata mrabaha stahiki na kodi kwa uwazi ili kuchangia pato la Taifa na kuimarisha ulinzi na usalama kwa wauzaji, wanunuzi na mali zao.

Minada kama hiyo pia hufanyika kwa nchi za Afrika zenye madini ya vito zikiwemo Zambia (emerald), Zimbabwe na Afrika Kusini (almasi).

Kulingana na taratibu za Tume ya Madini Tanzania, uboreshaji na utekelezaji wa kanuni za usimamizi wa masoko na vituo, minada ya ndani na kimataifa ya madini ya vito, itaendeshwa na tume hiyo kwa kushirikiana na Soko la Bidhaa la Tanzania (TMX), kupitia mfumo wa mauzo wa kielektroniki. uthaminishaji na upangaji wa madini ili kupata bei nzuri kulingana na madini husika.



Wananchi wa kijiji cha Moya Mayoka kata ya Magara wilayani Babati mkoani Manyara wakiwa eneo lililoathiriwa na kushuka kwa tope na mawe kutoka mlima Magara jana. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# JK kushiriki Rombo Marathon

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

RAIS mstaafu, Jakaya Kikwete ameahidi kushiriki mbio za hisani za Rombo Marathon Desemba 23, mwaka huu mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya kuchangia mradi wa upanuzi wa Hospitali Teule ya Huruma inayotarajiwa kupandishwa hadhi kuwa ya rufani. Jana, Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Raymond Mwangwala, alisema wanataka fedha zitakazopatikana katika mbio hizo zinazofanyika kuelekea sikukuu za Krismas mwaka huu na mwaka mpya wa 2025, zichangie mradi wa hospitali hiyo ili kuipandisha hadhi.

"Lengo letu sisi wana Rombo, tunataka matibabu yote tuwe tunayapata hapa mpaka ya rufani; ndio maana tumeamua tupeleke mchango wetu," alisema.

Alisema mbizo hizo za Rombo Marathon ni kwa ajili ya kurejesha kwa wananchi kile kilichopatikana na nguvu iliyotumika mwaka mzima irejee kwa wale wasio na uwezo.

"Kuwarejeshea wale ambao wana uhitaji na kusaidia jamii yetu kiujumla. Katika Marathon hii kile kiasi cha fedha kitakachopatikana, pia tunakipeleka kwenye ujenzi wa vyoo vya shule za msingi na sekondari," alisema.

Hospitali hiyo ambayo inamilikiwa na Kanisa Katoliki nchini, ilianzishwa mwaka 1968, ambapo 1972, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliridhia kupandishwa hadhi na kuwa Hospitali Teule ya Wilaya ya Rombo na baadae kuwa Hospitali ya Wakala wa Hiari.

Zaidi ya wakimbiaji 1,200 wanatarajiwa kushiriki mbio hizo, ambazo zinatarajiwa kuwavutia watu kati ya 3,000 mpaka 5,000.

"Msimu huu wa tatu tunatarajia kupata wakimbiaji 1,200, lakini kuna wakiambiaji ambao tunawaruhusu waje kupamba Marathon hii tunakadiria tuwe na watu zaidi ya 3,000," alisema mkuu huyo wa wilaya. Mwaka 2022, Mbunge wa Rombo na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolph Mkenda, akishirikiana na wafanyabiashara mkoani Kilimanjaro, walichangia zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura na uzio kuzunguka hospitali hiyo.

# Wafurahi kujengewa kivuko

**Na Mary Mosha,** SIHA

WAKAZI wa Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro wameonesha kufurahishwa na uamuzi wa serikali kuwaondolea kero ya kukosa kivuko eneo la Manyata kwa kuwajengea daraja.

Kabla ya serikali kujenga daraja hilo la Manyata, wakazi hao hususani wajawazito walikuwa wakijifungua kabla ya kufika hospitali na wengine kufa kwa kukosa huduma kutokana na kukosekana kwa kivuko.

Wakizungumza na Nipashe jana baada ya Bodi ya Barabara ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Mkoa wa Kilimanjaro, kukagua mradi huo, Fransia Laizer, alisema msimu wa mvua, walikuwa wanashindwa kufuata huduma za jamii upande wa pili.

"Binafsi mtoto wangu hakufanya mtihani wa darasa la nne mwaka 2022 kutokana na hali ya hewa. Niliogopa kumpitisha eneo hili; pia tumeshuhudia vijana wetu wengi, hasa waendesha pikipiki wakisombwa na maji na wengine kupoteza maisha wakati wakijitafutia riziki,"alisema Fransia.

Kuhusu ujenzi wa daraja la mawe la Manyata, Meneja TARURA wa Wilaya ya Siha, Protas Kavishe, alisema utagharimu Sh. milioni 336.9 zilizotolewa na serikali.

Kavishe, alisema hadi sasa ujenzi huo umefikia asilimia 92 na kwamba unatarajiwa kukamilika Januari 15 mwaka ujao.

Wakati Bodi hiyo ikiwa Wilaya ya Hai, baadhi ya wakazi wake walijitokeza kushuhudia ukaguzi huo, akiwemo Sendiki Mollel na kusema: "Tunaishukuru serikali kwa kusikia kilio chao cha ubovu wa miundombinu ya barabara ya Bomang'ombe/Kikavu Chini na kutopitika kwa Daraja Manyata nyakati za mvua. Sasa tutapeleka mazao yetu pamoja maziwa sokoni."

Meneja TARURA Wilaya ya Hai, Francis Kayu, akitoa taarifa ya ujenzi wa barabara ya Bomang'ombe /Kikavu Chini, alisema ulianza Agosti 5, mwaka huu na kutarajiwa kukamilika Agosti 4, mwaka 2025 kwa Sh. bilioni 2.8.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, aliwahadharisha makandarasi wazembe waliopewa zabuni mkoani humo kuwa hawatoongezewa mkataba na serikali.

Bodi hiyo, pia imetembelea ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ya Getifonga/Mabogini Kahe iliyopo Wilaya ya Moshi yenye urefu wa kilomita 1.2.

## TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Miaka 37 Bongo bila Nico Zengekala, aliyetuachia msamiati wa Solemba

**Na Adam Fungamwango**

JUMANNE ijayo, wadau na mashabiki wa muziki Afrika Mashariki, wataadhimisha miaka 37 ya kifo cha aliyekuwa mwanamuziki maarufu na mahiri wa bendi ya Juwata Jazz Band wakati huo, wana Msondo Ngoma.

Mwanamuziki huyu mwenye ulemavu wa macho, kwa muda mfupi tu alioingia na kufanya kazi ya muziki nchini akutoka Kenya, akipigia bendi mbili tu, za Les Cubano ya Morogoro, na Msondo Ngoma, aliondokea kuwa kipenzi cha wanamuziki wa dansi nchini, kutokana na umahiri wa kuimba, kutunga, ikiwemo sauti yake nyororo, laini, mwenyewe akiwa na uwezo wa kuitumia vyovyote atakavyo, wakati mwingine akitetemesha kama maji yanayotoririka kutoka kwenye milima.

Ni mwanamuziki ambaye kuanzia 1984, hadi kifo chake, alikuwa amejikusanyia mashabiki wengi na kuwa gumzo kiasi cha kuzima umaarufu wa wanamuziki wengi nchini Tanzania.

**KIFO CHAKE**

ILIKUWA ni saa tatu usiku ya Desemba 17, 1987, kwenye kipindi cha majira, ndipo mtangazaji alipowatangazia Watanzania kifo cha ghafla cha mwanamuziki maarufu sana wakati huo, Nico Zengekala.

Mtangazaji akasema, mwanamuziki huyo alifariki ghafla saa 11:00 alfajiri, nyumbani kwake Mtaa wa Sikukuu, Dar es Salaam.

Kilichotokea ni taharuki. Hakuna aliyeamini kuwa Nico, mwimbaji mwenye sauti tamu, nyororo ambaye ni mlemavu wa macho, amefariki. Mwanamuziki ambaye tayari alikuwa ameshajinyakulia mashabiki wengi nchini Tanzania, miaka michache tu tangu aingie nchini kutokana na umahiri wake wa kuimba, akitokea kwao Kenya.

Habari zaidi zinasema kuwa hadi saa sita usiku, kuamkia kifo chake alikuwa anapiga soga na marafiki zake mitaa ya nyumbani kwake, Kariakoo mtaa wa Sikukuu, Dar es Salaam ambako alipewa nyumba ya kuishi na bendi aliyokuwa anapigia ya Juwata Jazz, wana Msondo Ngoma.

Zilikuwa ni moja kati ya nyumba zinazomilikiwa na Juwata.

Kutokana na ustaa wake, na kifo chake cha ghafla, ilisababisha taharuki kubwa, vilio, simanzi, na kila aina ya huzuni ilitawala, Tanzania, Kenya na Uganda, huku baadhi ya Wabongo wakiwa hawaamini kama kilikuwa ni kifo cha kawaida.




Mwanamuziki Nico Zengekala akiwa kwenye steji ya Juwata Jazz, wana Msondo Ngoma katikati ya miaka ya 1980, alikuwa kwenye ubora wa hali ya juu.

Ni kifo kilichozua maneno mengi kuliko kawaida. Wengine wakasema ni mambo ya kishirikina. Wapo waliodai alilishwa sumu. Na wengine walisema umaarufu wake alioupata kwa muda mfupi tu, ulikuwa ni mwiba kwa wanamuziki si wa Msondo tu, bali hata wa Tanzania nzima, alioneka kuwafunika, hivyo baadhi yao hawakupendezewa. Lakini yote hayo yanamalizwa na ripoti ya madaktari kuwa alifariki kwa ugonjwa wa kifafa. Ndiyo uliomuondoa akiwa na umri kati ya miaka 20 hadi 24.

**NYIMBO ZAKE**

Alipoingia nchini na bendi ya Les Cubano, alitamba na vibao kama 'Jackie', 'Mwalimu Nyerere', 'Suzzy', 'Bwana Salim', 'Shemango', 'Mama Hisani' na nyingine nyingi.

Mwaka 1985 alichukuliwa na Msondo ngoma ambako nako alitamba na vibao kama 'Solemba' alichokitunga mwenyewe na vingine akiviimba kwa ustadi mkubwa kama 'Hasira Hasara', 'Kaka Mahmood', 'Asha Mwanasefu', 'Prisila', 'Kambarage Nyerere' na nyingine.

Wengi hawajui kuwa Nico Zengekala aliimba kwa umahiri mkubwa na kutunga nyimbo ambazo hadi anafariki alikuwa hajazirekodi. Nazo ni 'Dalila', huku akitunga 'Cha Mlevi hulikuwa na Mgema', pamoja na 'Razole' ambazo kama angebahatika kurekodi ingekuwa habari nyingine.

Hivi vyote awali ilikuwa virekodiwe na Nico, lakini alifariki kabla ya kwenda studio.

Kama nilivyosema, alikuwa na sauti tamu, nyororo, kali, ambayo alikuwa na uwezo wa kuitetemesha na, wakati mwingine akiishusha sauti kama mtu anayeweseka hivi.

**KUINGIA KWAKE NCHINI**

Alizaliwa katika kijiji cha Wundayi eneo la Mwatate karibu na mji wa Voi, kiasi cha kilometa 100 hivi kutoka Mombasa nchini Kenya.

Alichukuliwa na kuletwa nchini na mabaki wa wanamuziki wa Super Volcano ya Mbaraka Mwinshehe aliyefariki Kenya mwaka 1979, ambao baadhi walijiunga na Simba Wanyika, Les Wanyika, Wanyika Stars, Super Wanyika na Jobiso, ambao walimuona akiimba kwenye bendi moja ya Wataita wenzake Nairobi.

Wanamuziki hao ambao ni Watanzania waliokuwa nchini humo wakiendelea na shughuli za muziki, waliombwa kurejea nchini na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro wakati huo Nicodemus Banduka, hivyo wakaamua kumchukua Nico, ambapo yeye mwenyewe pia alitaka kuondoka Kenya.

Kwa mujibu wa mwanamuziki Said Makelele ni kwamba ilibidi kwenda kumuomba baba yake, ambaye aliwakubalia kwa madai kijana wake ameshindikana, kwani amemkataza sana mambo ya muziki, lakini amekuwa akitoroka nyumbani kwa kupasua dari juu, kwenda kuimba sehemu mbalimbali licha ya kumfungia na kufuli ndani. Baba yake aliwaambia kuwa akidhani amemfungia, lakini watu wanakuja kumwambia amemuona akiimba kwenye mabaa na kumbi mbalimbali, huku wakimsifia kwa uimbaji wake.

Makelele anasema ilibidi wadanganye ni Mtanzania ili aruhusiwe kuvuka mpaka wa Tanzania na Kenya, kwani wakati huo alikuwa na umri wa miaka 17, hivyo asingeweza kuruhusiwa kuvuka Wakadai ni Mtanzania wa Dodoma na wao ni wanamuziki wanaorejea nyumbani Tanzania kwa wito wa Mkuu wa mkoa wa Morogoro, ndipo waliporuhusiwa.

Inawezekana wakati anafariki huenda alikuwa hajafikisha hata miaka 24, na inawezekana Msondo walimpandisha umri ili aweze kuajiriwa na Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania JUWATA, kwani wasingeweza kumuajiri mtoto.

Ni kwa sababu kama aliingia nchini ana miaka 17 na hakudumu na bendi hiyo kwa zaidi ya miaka miwili akajiunga na Msondo.

Ni mwanamuziki aliyedumu kwa muda mfupi nchini, lakini sauti na uimbaji wake hadi leo hi umeendelea kuwa lulu na wimbo wake wa 'Solemba' na msamiati ukiendelea kuishi.

Hakuwa staa kwao Kenya, lakini nyota ilimuwakia nchini na hata mwili wake uliposafirishwa, ulikuwa ni msafara na heshima kubwa wa magari lukuki ya serikali ya Tanzania, Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania, Chama cha Muziki wa Dansi Tanzania (Chamudata), wapenzi na mashabiki kama vile anayekwenda kuzikwa ni kiongozi mkubwa wa kitaifa.

Hii iliwashangaza na kuwaliza wengi kwao, zaidi wazazi na ndugu zake, kwani aliondoka akiwa wa kawaida tu, lakini maiti yake imerudishwa nyumbani kishujaa. Hawakuamini.

Alizikwa kijijini kwao Wundayi, Mwatate, Voi, Taveta nchini Kenya Desemba 24, 1987.

Huyo ndiyo Zengekala, mwimbaji 'kipofu', kutoka Kenya, aliyeacha simulizi isiyofutika Tanzania.

**Tuma meseji 0716 350534**

## Trump apinga makombora yao kushambulia Russia

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS mteule wa Marekani, Donald Trump, amesema hakubaliani na suala la Ukraine kurusha makombora yaliyotolewa na Marekani ndani ya ardhi ya Russia.

Katika mahojiano yaliyofanyika Alhamisi ya wiki hii, Trump alisisitiza kuwa Marekani haitaiacha Ukraine na itaendelea kuinga mkono.

Amesema njia atakayoichukua ni njia katika juhudi za kumaliza vita.

Washington imepeleka makombora ya masafa marefu ya ATACMS nchini Ukraine ambayo yanaweza kupenya ndani ya Russia.

Hata hivyo, Ukraine imetumia makombora hayo kufanya mashambulizi kadhaa na kusababisha ulipizaji kisasi kutoka kwa Russia kwa kutumia kombora jipya hypersonic.

"Napinga vikali kupeleka makombora mamia ya maili nchini Russia. Kwa nini tunafanya hivyo?" alihoji Trump katika mahojiano na jarida la Time ambalo lilimtaja kama mtu bora wa mwaka.

Makombora ya ATACMS yana uwezo wa juu wa kushambulia maili 190 sawa na kilomita 300 kulingana na data iliyotolewa kwa umma.

**BBC**

## Marais Rwanda, DRC kukutana kesho Angola

**LUANDA,** ANGOLA

MARAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) Felix Tshisekedi na Rwanda, Paul Kagame wanatarajiwa kukutana kesho nchini Angola kujadili amani.

Mkutano huo ni awamu mpya ya mazungumzo yanayodhamiria kuumaliza mzozo wa mashariki mwa DRC.

Rwanda imethibitisha ushiriki wa Kagame atakayeambatana na Waziri wake wa Mambo ya Nje Olivier Nduhungirehe.

Kwa upande wa DRC ilithibitisha, Rais Tshisekedi atahudhuria mazungumzo hayo licha ya hapo awali kukataa kuzungumza na Rwanda.

**DW**

# Marekani yaona matumaini kusitishwa mapigano Gaza

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imesema ina matumaini ya kuafikiana makubaliano ya kusitisha mapigano ya Gaza hivi karibuni.

Hata hivyo, Israel iliendelea kufanya mashambulizi dhidi ya maeneo kadhaa ya Ukanda wa Gaza na kuua zaidi ya Wapalestina 60 ndani ya saa 24.

Akizungumza wakati akiwa kwenye ziara nchini Uturuki jana, Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Marekani, Antony Blinken, alisema alikuwa anaona dalili za kuelekea makubaliano ya kusitisha mapigano Ukanda wa Gaza ambao umeteketezwa kwa makombora na mizinga ya Israel.

"Tumejadili kuhusu Gaza, na tumejadili fursa iliyopo ya kupata makubaliano ya kusitisha mapigano. Na tumeona kwamba ndani ya wiki chache zilizopita, kumekuwa na ishara za kutia moyo kwamba jambo hilo linawezekana."

Alisema Blinken baada ya mazungumzo na mwenyeji wake, Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Uturuki, Hakan Fidan.

Kumekuwapo na uvumi kutoka Marekani kwamba rais mteule wa Marekani, Donald Trump, ameagiza suala la Gaza liwe limemalizika kabla ya yeye kuingia rasmi madarakani mwezi ujao, hali inayoashiria kwamba wapatanishi wa kimataifa pamoja na pande zote zinazohusika na hali inayoendelea Gaza wana muda wa chini ya wiki tatu kuhakikisha vita vinasitishwa.

Marekani pamoja na mataifa kadhaa ya Magharibi yamekuwa vinara wa uungaji mkono wa kijeshi, kifedha na kisiasa kwa Israel.

Hali katika Gaza, inaelezwa mashambulizi ya anga ya Israel yamewauwa Wapalestina 30 na kuwajeruhi wengine wapatao 50 usiku wa kuamkia jana pekee.

Aidha, familia kadhaa ambazo zimegeuka kuwa wakimbizi wa ndani kutokana na miezi 14 ya mashambulizi, zilikuwa zimejihifadhi kwenye jengo moja la huduma za posta katika kambi ya wakimbizi ya Nuseirat.

Mashambulizi hayo yaliifanya idadi ya waliouawa kwa siku nzima ya jana kufikia 66.

Jeshi la Israel lilidai kwamba mashambulizi hayo yalimlenga mwanachama wa ngazi za juu wa kundi la Islamic Jihad, mojawapo ya makundi yaliyohusika na uvamizi uliofanyika Oktoba 7 mwaka jana ndani ya Israel.

Hata hivyo, Israel haikulitaja jina la mwanachama huyo wa Islamic Jihad ambaye inadai anahusika na mashambulizi dhidi ya raia na wanajeshi wake.

Hata hivyo, ilisema kundi hilo linatumia miundombinu ya raia na wakazi wa Gaza kama ngao kwa harakati zake.

Kambi ya wakimbizi ya Nuseirat ni mojawapo ya kambi nane za kihistoria kwenye Ukanda wa Gaza ambazo zimekuwa zikiwahifadhi Wapalestina tangu mwaka 1948.

Kambi hiyo kwa sasa, ni sehemu ya mojawapo ya maeneo yenye idadi kubwa ya watu, baada ya maelfu ya waliokimbia maeneo mengine ya Ukanda huo kwenda kujihifadhi.

**DW**



Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken (kushoto) akizungumza na Rais wa Uturuki Recep Tayyip Erdogan jijini Ankara, nchini Uturuki jana. Viongozi hao walijadili hali ya kisiasa nchini Syria. **PICHA: ALLIANCE**

# Odinga aanza mchujo AU

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

MWANASIASA mkongwe kutoka Kenya, Raila Odinga, ameshiriki mdahalo na wagombea wengine wawili kujiandaa na kinyang'anyiro cha kumchagua mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika.

Mdahalo huo ambao ulifanyika jana saa 1:00 jioni kwa saa za Afrika Mashariki, utatoa nafasi kwa wagombea hao kuonesha uwezo wao wa kutumikia nafasi hiyo kubwa katika Umoja wa Afrika.

Mdahalo huo kuhusu Afrika utafanyika katika makao makuu ya Umoja wa Afrika (AU) yaliyoko mjini Addis Ababa, nchini Ethiopia.

Kwenye mdahalo huo Raila atakuwa pamoja na wagombeaji wengine wawili, akiwamo Waziri wa Mambo ya Nje wa Djibouti, Mahamoud Ali Youssouf na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Madagascr, Richard Randriamandrato.

Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Mauritius Anil Kumarsingh Gayan, alijiondoa katika uchaguzi huo mapema mwezi huu.

AU ilisema Mdahalo wa Afrika ni jukwaa la wagombea kuhutubia raia wa Afrika katika mdahalo wa televisheni, unaorushwa moja kwa moja.

Wagombea watawasilisha maono na mawazo yao juu ya utekelezaji wa Ajenda ya 2063 ya umoja huo.

"Mjadala unaangazia masuala ya sera na ushiriki wenye mwelekeo wa kupata suluhu kuhusu kila mgombea anavyopanga kuendeleza matarajio na malengo ya ajenda ya 2063, miradi mingine ya AU yenye mwelekeo wa bara, na msimamo ya pamoja ya Afrika," ilisema taarifa ya AU.

**BBC**

# TPSF yabadilika kutoka taasisi kuwa shirikisho

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imefanya mageuzi makubwa kwenye katiba yake ili kuendelea kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi na kuanzia sasa itatambulika kama shirikisho.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Raphael Maganga (pichani), alisema hayo juzi alipofanya kikao na wahariri na waandishi wa habari ofisini kwake, Dar es Salaam.

Alisema maboresho hayo yalipitishwa na mkutano mkuu wa wanachama uliofanyika Novemba 20, mwaka huu, na kwamba ulihudhuliwa na zaidi ya asilimia 70 ya wajumbe halali wa TPSF na ajenda ilikuwa kufanya maboresho kwenye katiba.

Maganga alisema maboresho hayo yalilenga kuongeza ushiriki wa kongani ambazo hazikuwepo kwenye mfumo wa TPSF, kuimarisha sauti na ushawishi wa sekta binafsi na wafanyabiashara nchini kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa na taifa hivyo kuhakikisha uboreshwaji wa mazingira ya biashara nchini.



Alisema maboresho hayo yalitokana msukumo mkubwa kutoka kwa wadau wa sekta binafsi ambao hawakuwa na uwakilishi TPSF na msukumo ulitokana na ukuaji mkubwa wa sekta binafsi ndani ya miaka ya hivi karibuni ambayo imechangia sana ukuaji wa vyama nchini.

Maganga pia alisema maboresho hayo yalifanywa kuzingatia maazimio ya vikao vya Baraza la Taifa la Biashara ambayo pamoja na mambo mengine, Rais Samia Suluhu Hassan, alilisitiza taasisi za sekta binafsi nchini ziimarishe uhusiano miongoni mwa wadau wa sekta binafsi na taasisi zao zishirikiane na kuimarishe miiko na maadili ya sekta binafsi.

"Hivyo kama TPSF tuliona agizo la Rais ni muhimu sana katika kuhakikisha sekta binafsi nchini ina uratibu madhubuti wa vyama vya biashara, inakuwa sekta inayotii sheria na yenye nidhamu," alisema.

Maganga alisema katika maboresho hayo wameamua kuwa kuanzia sasa TPSF itajulikana kama Shirikisho la Sekta Binafsi Tanzania na kwamba mabadiliko hayo yamefanywa ili kuondoa mkanganyiko uliokuwapo kati ya wadau kuwa taasisi hiyo ni shirika la kutoa misaada.

Alisema ili kuhakikisha kuna mfumo shirikishi, Shirikisho limeongeza wawakilishi na makundi muhimu ambayo hapo awali hayakuwepo kama vile Wanawake, Biashara za vijana, ufugaji, uvuvi, afya, elimu, michezo, ubunifu, teknolojia na mawasiliano, uchumi wa kidijitali pamoja na kuongeza uwakilishi kutoka Zanzibar.

# Wananchi walalamikia kero kiwanda kutiririsha majitaka

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

WAKAZI wa Mtaa wa Vitendo Kata ya Misugusugu, Halmashauri ya Mji wa Kibaha mkoani Pwani wamelalamikia kiwanda kinachozalisha kemikali za kutengenezea pombe kali kutiririsha maji machafu yenye harufu kali yanayopita katika makazi ya watu na mashamba.

Maji hayo yanadaiwa kuleta madhara kwenye mashamba ambayo yalikuwa yanalimwa mpunga na kusimamisha shughuli za kilimo, huku harufu kali ikiwa kero nyakati zote kwa wanaoishi karibu na kiwanda hicho.

Kuwapo kero hiyo kulianza kuelezwa na Mchungaji Sixtus Malya katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha kilichofanyika hivi karibuni kikiongozwa na Mwenyekiti ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson John.

Malya alieleza namna wananchi wanavyotaabika na maji hayo huku waliokuwa wakifanya shughuli za kilimo kusimama kutokana na uwingi wa maji hayo meusi yanayoua mimea.

Nipashe ilifunga safari mpaka eneo hilo ikianzia kwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Vitendo na baadaye kufika kwenye maeneo yanayotiririsha maji hayo kutoka kiwandani ambapo kuna mabomba yaliyoelekezewa shambani.

Maji machafu yanayotiririka kutoka kiwandani yamewekewa mabomba ambayo yanaelekea kwenye mashamba ya wananchi na bonde walimokuwa wakitumia wakazi wa eneo hilo kwa kilimo cha mpunga ambalo lipo jirani na makazi ya watu.

Wakizungumzia kuhusiana na kero hiyo baadhi ya wakazi wa eneo hilo la kiwanda akiwemo Ditrick Haule, Juma Meena, Winning John na Mwamvuta Shubet walisema malalamiko yao wamekuwa wakiyafikisha kwa viongozi lakini bado hayajapatiwa ufumbuzi.

Haule alisema maji hayo machafu yameathiri maeneo yao ya kilimo na kwamba mbali ya mabomba yaliyoelekezewa bondeni pia wakati mwingine kuna magari ya kiwanda hicho yamekuwa yakibeba maji machafu kutoka kiwandani na kuyamwaga barabarani.

"Huo udongo mweusi unaouona umebadilishwa na .amani yanayobebwa na mabomba ambayo yanamwagwa barabarani yanaacha harufu kali, lakini pia yakimwagwa kwenye majani yanaungua hakuna kitu kinaota hapo," alisema.

Naye, Juma Meena alieleza kwamba endapo angekuwa na uwezo wa kuuza eneo lake angefanya hivyo ili kuondokana na kero ya harufu kali wanayokunbana nayo.

Winni John alisema katika eneo hilo wanakosa hewa safi kutokana na harufu kali zinazotoka kwenye maji yanayotiririka sambamba na kelele ambazo zinawaathiri wanafunzi Shule ya Sekondari Misugusugu iliyokaribu na kiwanda hicho.

Bahati Mbaigwa ameomba serikali kuingilia kati ikiwezekana kuhamisha shule hiyo kwani wanafunzi wanaosoma katika shule hiyo wakati mwingine wanashindwa kuhimili harufu kali wakiwa darasani.

"Ikiwezekana shule ihamishwe kiwanda kibaki kwani wanafunzi wanathirika na kelele za kiwanda na harufu na hii inawasababishia kutokuwa na utulivu wakiwa darasani, "alisema.

Mmoja wa wananchi wa Mtaa wa Vitendo ambaye hakutaka kutajwa jina lake alisema wapo wananchi wanaumwa koo na wanafunzi wengine wanaomba kuhama kutokana na kushindwa kuhilimi kero zinazotokana na kiwanda hicho.

"Wazazi wengine hawataki kupeleka watoto wao katika shule hiyo na baadhi yao wanawahamisha watoto wao kutokana na harufu kali ambayo inawaumiza wanafunzi na wakati mwingine kelele ze kiwanda zinafika moja kwa moja wanashindwa kusikilizana darasani, " alieleza.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Vitendo, Ally Lunga alithibitisha kuwapo malalamiko hayo kutoka kwa wananchi huku akiomba kiwanda hicho kufanya marekebisho ya kuondoa harufu na kuweka mfumo wa utirishaji maji yanayotoka kiwandani.

Akiwa katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson John alikiri kufahamu kero ya kiwanda hicho huku akiahidi kuwa wilaya inalisughulikia ili kumaliza tatizo hilo.

Mwandishi aliutafuta uongozi wa kiwanda, lakini haukuwa tayari kuzungumzia hatua walizochukua kukabiliana na hali hiyo.

# Walemavu wafunzwa urejeshaji wa mikopo

**Na Hamida Kamchalla, TANGA**

BAADHI ya watu wenye ulemavu mkoani hapa wanashindwa kurejesha mikopo ya asilimia mbili kwa halmashauri kwa kukosa elimu ujasiriamali na kulipa kodi, imebainika.

Mwenyekiti wa Umoja wa Miradi kwa Viziwi Tanzania (UMIVITA), Ally Nassoro, alitoa siri hiyo jizi wakati wa mafunzo ya elimu ya mlipa kodi kwa kundi hilo yaliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani hapa.

Nassoro alisema mikopo hiyo inawasaidia kuendesha biashara na kujikwamua na umasikini, wengine wanafanikiwa kurejesha na baadhi kushindwa huku wakikimbia makazi yao kukwepa kudaiwa.

"Wanaoshindwa kurejesha wanawanyima wenzao haki ya kupata mkopo, sheria ya mkopo inasema kopa halafu rejesha," alisema na kuwasisitiza ambao wanadaiwa walipe ili kutoa fursa kwa wengine kukopeshwa.

Akizungumzia kuhusu elimu hiyo waliyopatiwa na maofisa wa mamlaka hiyo, alisema itawanufaisha kwa kuongeza mitaji na kulipa kodi.

"Tumefurahi kupata elimu hii itatusaidia kufuatilia ulipaji kodi kwa wakati," alisema.

Ofisa Mkuu Msimamizi wa Kodi Elimu kwa Mlipakodi na Mawasiliano Tanga, Flavian Byabato, alisema kwa kushirikiana na UMIVITA wametoa elimu hiyo kwa kundi hilo ili kuwaongezea uelewa.

Byabato, alisema elimu waliyotoa ni pamoja na usajili wa biashara na kulipa kodi.

"Lakini wana haki ya kupewa hati safi ya ulipaji kodi baada ya kukamilisha taratibu ikiwemo matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki (EFD) na utoaji wa risiti," alisema.

Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) Mkoa wa Tanga, Subira Hoza, alisema kabla ya kupata elimu hiyo watu wenye ualbino mkoani humo walikuwa wanafahamu kuhusu elimu ya mlipa kodi kwa asilimia 30.

"Lakini leo tumejifunza mambo mengi sana, hasa kuhusu ulipaji kodi kwa mtu mwenye kupata kiwango cha juu na chini na misamaha ya kodi," alisema.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.
Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-43

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Ghafla Kamal akajikuta amekumbatiwa kwa nguvu na mtu ambaye hamfahamu. Hata hivyo mtu aliyemkubatia alionekana kuwa na mwili laini uliomfariji kwa kiasi fulani.

"Shemeji Kamal." Ilisikika sauti ambayo iliita jina lake na kulia. Mtu aliyemkubatia na kuanza kuangua kilio ni Teddy. Huyu ni mdogo wa marehemu Mariamu. Kumbe naye alikuwa mahakamani. "Teddy!" akaita Kamal.

"Nilijua na wewe umekufa shemeji yangu!" Aliendelea kulia. ""Nyamaza Teddy, isingewezekana kufa kabla sijatimiza ahadi yangu niliyoiweka. Nilikwambia siku ile wakati nakuaga kuwa ni lazima nimpate muuaji wa dada yako Mariamu. Na nyingine unaijua mwenyewe." Maneno hayo yalimfanya Teddy kwanza anyanyue kichwa na kumtazama Kamal, lakini kwa aibu kwani macho yake yalishindwa kuendelea kutazama zaidi.


"Umekuja na nani?" "Nimekuja na ndugu zangu wote." "Mbona hawakuja kuniona." "Shemeji wewe mwenyewe unajua kilichotokea nyuma. Wale wote walikuwa wanakushutumu na kukuhisi kuwa wewe ni kweli umemuua dada kama ambavyo askari walivyobainisha. Unajua ni mimi peke yangu nilikuwa siamini na nisingeamini kamwe. Na nilipata lawama na kutoaminiwa na ndugu zangu kwa sababu hii ya kukutetea, leo ukweli umedhihirisha tena ni wewe mwenyewe ndiye uliyekuwa ukisaka ukweli. Haiwezekani kirahisi zaidi waje hapa. Bado wana aibu. Itachukua muda kidogo.

"Basi mama, ngoja niondoke na hawa jamaa zangu. Baada ya siku mbili nitakutafuta nina kesi na wewe ujue."

Teddy akatabasamu. Akamuacha Kamal aliyekuwa amemkumbatia. Akaachia tabasamu zito wakati bado machozi yalikuwa hayajakauka mashavuni.

********************************************

"Nimekuiteni hapa kwa sababu moja au mbili hivi. Nimepata taarifa kutoka kwa IGP, kuwa hivi karibuni atatangaza kukupandisha cheo afande Willy na hapo hapo kukupeleka kwenye mafunzo ya ukachero ya miezi sita nchini Urusi. Kamanda wa Polisi Kanda Maalum alimwambia Willy aliyekuwa amekaa kulia, huku rafiki yake Kamal akiwa upande wa kushoto. "Hii ndiyo taarifa nakupa, na siku hiyo mtakuwa askari polisi 50 ambao mtapandishwa cheo kwa ngazi mbalimbali na kutunukiwa nishani. Wewe utapandishwa cheo na kutunukiwa nishani iliyopewa jina la shujaa wa jamii. Yaani umeikosha jamii. Umewafurahisha raia. Wakati watu wote, pamoja na Jeshi la Polisi kuamini kuwa muuaji wa Mariamu ni mpenzi wake na kuanza kumsaka, wewe umekuja na kitu tofauti na kumuibua kutoka kusikojulikana muuaji halisi. Inawezekana hakuna ambaye angeweza kukubali kama si ushahidi usio shaka ambao uliutafuta kwa akili, juhudi, ufundi, ubunifu, nguvu na ustadi wa hali ya juu kiasi kwamba hata mahakama haikupata shida kuendesha kesi hii na kuwatia hatiani watuhumiwa.




**"Dada aliyekwambia wewe utaanza kufa kabla ya mimi nani? Ushaanza hivyo, hapa tuko kwenye furaha unaanza mambo yako."**

IGP, amesema ubunifu na uwezo uliooonyesha, ukiongezwa na mafunzo, basi unaweza kulisaidia taifa kupambana na maadui wetu," alisema Kamanda. Akanyamaza. Akayaondoa macho kwa afande Willy na kumkazia Kamal.

"Hukuwa askari polisi. Ulituhumiwa kumuua mpenzi wako. Siyo kimakosa bali kwa makusudi na watu ambao walitumia uwezo wao wa kifedha kuwaaminisha mpaka polisi wetu kuwa ni kweli umefanya hivyo.

Ukaamua kutoroka na kujificha. Hukujificha tu ili usikamatwe bali ulikuwa na kazi moja tu ya kumsaka muuaji halisi kwa sababu uliamini kuwa wewe siyo, licha ya wananchi kuaminishwa hivyo. Ulibebwa na woga wa kukamatwa kwa kubambikiwa kesi isiyo yako, lakini pamoja na uchungu wa kuuawa kwa mpenzi wako, ukatumia mbinu na ujanja, uwezo uliokuwa nao ili kumsaka muuaji halisi. Kwa kushirikiana na afande Willy, mkafanikiwa kufanya kitu ambacho hufanywa na makachero na wapelelezi wenye uwezo wa hali ya juu, mpaka kufanikiwa mlichofanikiwa. Kwa maana hiyo, IGP, ameagizwa wewe usiachwe. Kwa sababu umri wako bado unaruhusu, utapelekwa kwenye mafunzo ya Jeshi la Polisi na baada ya miezi mitatu, na wewe pia utakwenda nchini Urusi kwa mafunzo ili kuwapata vijana shupavu ambao ni makachero." Vijana wote wawili walinyanyuka na kumpa mkono Kamanda wa Polisi Kanda Maalum na kushukuru.

"Kuna wahafidhina walisema kuwa afande Willy hukustahili kwa sababu ulifanya kazi bila ruhusa ya Jeshi la Polisi, hivyo unastahili adhabu, wakubwa tukakaa tukasema kuwa haistahili adhabu ingawa ni kweli umefanya hivyo, lakini umefanya kwa manufaa ya taifa na jamii kwa ujumla. Kama wewe tutakuadhibu kwa kazi hii, je wale waliokula rushwa na kutuaminisha kuwa Kamal amemuua mpenzi wake na taifa likakubali, wale walifanya kazi kwa kuagizwa na nani? Nawatakia kila la heri vijana wangu kwa majukumu mapya mtakayopewa na taifa, naamini hamtaniangusha mimi kwa sababu mmenipatia sifa sana, lakini msiliangushe taifa," akamaliza kamanda kwa maongezi ya kikazi, ukabaki utani tu baina yao.

************************************

"Waooo jamani karibu shemeji." Teddy akamlaki mgeni wake ambaye alimpigia simu kuwa atafika majira ya saa tano asubuhi siku ya Jumamosi hiyo.

Hakwenda kazini siku hiyo, ilikuwa siku yake ya mapumziko. Alikuwa ameanza kazi miezi mitatu iliyopita kwenye Hospitali ya Amana, Dar es Salaam, hivyo aliondoka kwa mama yake mkubwa alikokuwa amekaa na sasa alikuwa amepanga Chang'ombe maduka mawili.

Akamkumbatia na kumuingiza sebuleni kwake. "Karibu shemeji huku ndiko nakoishi siku hizi.

Wakati wanazungumza. Akili ya Kamal iliendа mbali sana. Alimkumbuka Mariamu mpenzi wake. Siku zote wakati yupo hai alikuwa akiwaambia kuwa wamefanana sana kama mapacha. Lakini kumbe ni mtoto wa mama mkubwa na mdogo. Teddy alijua hilo. Kwa sababu kuna wakati wanazungumza, halafu anamwangalia usoni mpaka akajisahau. Anakuwa hazungumzi tena mpaka Teddy anapomshtua. Wote wawili wakakumbuka mazungumzo ya zamani waliyokuwa wakizungumza wakati Kamal mwenyewe alipokuwa akiwachukua mpenzi wake Mariamu na Teddy kwenda kula chakula cha jioni, au kuwatoa 'auti'.

Kamal alikuwa anapenda mno kumtania. Alimwita mke mdogo. Mariamu alizaliwa na mama mkubwa, Teddy mdogo, ambapo mama zao walizaliwa tumbo moja.

Kamal alimzoea zaidi Teddy kuliko ndugu wengine. "Yaani mmefanana na dada yako kama korosho." Kamal alikuwa akimtania Teddy.

"Ikitokea bahati mbaya nikifa, muoe Teddy, mimi nitakuwa radhi kabisa, lakini ukioa mwanamke mwingine nitakutokea usiku wewe na huyo mkeo." Ni maneno aliyokuwa akiyaongea Mariamu mara kwa mara, anapokuwa na Kamal pamoja na Teddy.

Hakuna aliyekuwa akiyatilia maanani kwa sababu yalionekana ni kama maneno ya utani na kunogesha stori.

"Dada aliyekwambia wewe utaanza kufa kabla ya mimi nani? Ushaanza hivyo, hapa tuko kwenye furaha unaanza mambo yako."

"Nasema ikitokea, sisi binadamu, huoni tulivyofanana, Kamal akiwa na wewe ataona kama yupo na mimi tu." Mariamu aliendelea.

"Teddy, achana na dada yako, anatuvuruga tu hapa, ukianza kuolewa kabla yeye hajafa halafu baadaye akifa na wewe upo kwenye ndoa, nitaachanisha ili nimuoe?"

Hayo ni maongezi ya mara kwa mara ambayo huongelewa pale, Kamal anapokuwa pamoja na ndugu hao wawili, Mariamu na Teddy, ambapo huwachukua na kwenda nao kula bata, mwenyewe aliwaita wake zake, Mariamu mkubwa, Teddy mdogo.

***Itaendelea Jumamosi***



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania ya Wasichana chini ya miaka 15 wakionesha medali baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye mashindano ya Shule ya Afrika kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CAF CECAFA U-15) yaliyomalizika nchini, Uganda juzi. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# PAWASA SASA AUTAMANI UBINGWA CECAFA U-17

**Na Mwandishi Wetu, KAMPALA**

BAADA ya kutwaa ubingwa wa mashindano ya U-15, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya vijana chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), Boniface Pawasa, amesema sasa wanajipanga kuhakikisha Tanzania inatwaa na ubingwa michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-17).

Mashindano hayo ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON U-17), yanatarajiwa kufanyika kuanzia kesho kwa kushirikisha nchi sita.

Nchi zilizothibitisha kushiriki mashindano hayo ni wenyeji Uganda, Tanzania, Kenya, Somalia, Sudan na Sudan Kusini.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa, Pawasa, alisema wako kamili kutetea ubingwa wa michuano hiyo ili kuendeleza rekodi nzuri ya kushiriki fainali hizo mfululizo. Pawasa alisema mashindano hayo yanatarajiwa kuwa magumu lakini maandalizi waliyofanya yanawaweka kwenye nafasi nzuri ya kupeperusha vyema bendera ya nchi.

"Tumekuja kupambana, tunajua hakutakuwa na mechi rahisi, kila timu inataka kushiriki AFCON, kwetu kila mechi sawa na fainali," alisema beki huyo wa zamani wa Simba, APR ya Rwanda na Taifa Stars.

Aliongeza kila mchezaji wa timu hiyo yuko tayari kwa mapambano na anafurahishwa na ushindani wa kuwania namba wanavyoonyesha wanapokuwa mazoezini. Serengeti Boys iliyoko Kundi A itaanza kampeni ya kuwania taji hilo kesho kwa kucheza dhidi ya Uganda wakati mechi ya mapema itawakutanisha Somalia na Sudan Kusini. Desemba 18, mwaka huu Serengeti Boys itakutana na Kenya na timu mbili zitakazofanya vizuri zitatinga hatua ya nusu fainali itakayochezwa Desemba 24, mwaka huu.

Kundi B la mashindano hayo linaundwa na Somalia, Sudan na Sudan Kusini wakati fainali za mashindano hayo zimepangwa kufanyika Desemba 27, mwaka huu.

# Hizi hapa timu zilizotinga raundi ya nne Kombe la FA

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya timu tisa za Ligi Kuu na 10 za Ligi ya Championship zimetinga hatua ya raundi ya nne ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), maarufu kama Kombe la FA zilizochezwa kwa siku tofauti wiki hii.

Jumla ya michezo 19 imechezwa, kasoro timu za Simba na Yanga ambazo zipo kwenye hekaheka ya michezo ya kimataifa.

Mechi hizo ni za kusaka ubingwa kwa ajili ya kucheza michezo ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika msimu ujao.

Tukianza na timu 10 za Championship zilizotinga raundi ya nne ni Transit Cam, Biashara United, Songea United, Cosmopolitan, Stand United, Mbeya City, Green Warriors, na TMA ambazo zote zilipata ushindi kwenye michezo yao ya mwisho

Kwa upande wa timu za Ligi Kuu zilizotinga hatua hiyo ni, Singida Black Stars, Mashujaa, Pamba Jiji FC, Coastal Union, Azam FC, Namungo na JKT Tanzania.

Klabu za Simba na Yanga zenyewe zitapangiwa michezo yao baada ya kumaliza majukumu ya michezo ya kimtaifa wa Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho wanayoshiriki kwa sasa wakiwa kwenye hatua ya makundi.

# Kocha Mashujaa alia joto Dar kuwakosesha ushindi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mashujaa FC, Mohamed Abdallah 'Bares', amesema kuwa joto kali la Dar es Salaam, ni moja kati ya sababu zilizosababisha timu yake ishindwe kupata ushindi dhidi ya KMC juzi katika mchezo wa Ligi Kuu.

Akizungumza mara baada ya kumalizika kwa mchezo huo, kwenye Uwanja wa KMC Complex, timu hizo zilitoka suluhu, Bares alisema hali ya hewa kwa kiasi kikubwa imewaathiri mno wachezaji wake kiasi cha kushindwa kucheza kwenye kiwango chao kilichozoeleka.

"Hali ya hewa imewaathiri sana wachezaji wangu, Dar es Salaam kuna joto kali sana kipindi hiki, sisi tumetoka Kigoma ambako kuna hali ya hewa nyingine kabisa tofauti na hii, lakini pamoja na hayo nashukuru wamecheza vizuri, ila siyo kwa kiwango ambacho nilitarajia.

Kipindi cha kwanza hatukucheza vizuri kabisa, hatukuwa kwenye muunganiko wetu, tulifanya mabadiliko tukapata pointi moja, ligi ni ngumu ukipata pointi moja ugenini shukuru Mungu, tunakwenda kujipanga," alisema Bares.

Naye Kocha Mkuu wa KMC, Kalimangonga Ongalla, aliia na wachezaji wake kukosa uzoefu kwani ilitakiwa waimalize mechi mapema tu.

"Tumetengeneza nafasi nyingi lakini tukashindwa kuzitumia, ila kiuchezaji nimeridhishwa, tatizo la timu yangu ni wachezaji wangu wengi kutokuwa wazoefu, kuna wakati tulikuwa tunatupa mpira kirahisi, kuna vitu bado natakiwa kuvirekebisha kwenye uwanja wa mazoezi," alisema kocha huyo.

Matokeo hayo, yanaipeleka Mashujaa kwenye nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikifikisha pointi 18 kwa michezo 13, huku KMC ikishuka hadi nafasi ya 11 ikiwa imeshacheza michezo 14, ikibakisha mmoja tu imalize mzunguko wa kwanza, imekusanya pointi 15 mpaka sasa.

## ZISIKUPITE

### VLAHOVIC AGOMBEWA

ARSENAL, Chelsea na Manchester United bado wanavutiwa na Dusan Vlahovic, huku Juventus wakifikiria kumuuza mshambuliaji huyo wa Serbia mwenye umri wa miaka 24, isipokuwa kama atakubali mkataba mpya. ***(TBR Football)***

### SALAH, LIVER WAMALIZANA

LIVERPOOL imetoa ofa ya mkataba mpya kwa mshambuliaji wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 32. ***(Athletic)***

### DIJK NAYE AKUBALI KUBAKI

LIVERPOOL pia wanatazamia kuwafunga beki wa kati wa Uholanzi, Virgil van Dijk mwenye umri wa miaka 33, na mlinzi wa kulia wa England, Trent Alexander-Arnold mweye umri wa miaka 22, kwa mikataba mipya. ***(Star)***

### ZUBIMENDI AWINDWA EPL

KLABU ya Manchester City inaweza kuharakisha kuipiku Liverpool katika mpango wa kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25, kutoka Real Sociedad. ***(Football Insider)***

### CHERKI AOTA MBAWA

JITIHADA ZA Crystal Palace kumsajili winga wa Lyon, Rayan Cherki mwenye umri wa miaka 21 zimezuiliwa na wababe wa Ulaya PSG pamoja na Borussia Dortmund waliojiunga katika kinyang'anyiro hicho. ***(Sun)***

### YILDIZ AWANIWA A' VILLA

KLABU ya Aston Villa ni moja kati ya klabu nne za Ligi Kuu ya England zinazomtaka winga wa Juventus na Uturuki, Kenan Yildiz mwenye umri wa miaka 19, ambaye klabu yake inaweza kumuuza kwa takriban pauni milioni 66. ***(BirminghamLive)***

### CHUKWUEMEKA NA MILAN

AC Milan ina nia ya kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea, Carney Chukwuemeka mwenye umri wa miaka 21, ambaye pia anawavutia Celtic. ***(Soccer Italia)***

### ENDRICK KUBAKI MADRID

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid mwenye umri wa miaka 18, Endrick ameamua kutoondoka kwa mkopo Januari na ataendelea kupigania namba kwenye timu hiyo. ***(Marca)***

### KVARATSKHELIA KUONGEZA

WINGA wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 23 anakaribia kusaini mkataba wa nyongeza na Napoli hadi 2029. ***(Corriere dello Spori)***

### ALLEGRI HAKIELEWEKI W'HAM

KLABU ya West Ham ilimchukulia Massimiliano Allegri kama mrithi wa kocha wa sasa Julen Lopetegui, lakini mahitaji yake ni makubwa mno. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RAPHINHA AWATOA HOFU BARCA

**Kocha Flick amethibitisha nyota huyo hajaumia bali alitolewa baada ya....**

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick ameondoa wasiwasi alipoulizwa kuhusu hali ya Raphinha baada ya ushindi wa Jumatano kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Dortmund.

Raphinha alikuwa nahodha wa Barca na kufunga bao katika ushindi wa mabao 3-2 kwenye Uwanja wa Signal Iduna Park na kuendeleza ubora wake wa kipekee.

Mbrazil huyo alikuwa na hofu ya nafasi yake msimu huu kutokana na klabu hiyo kumsaka hadharani mshindi wa Euro 2024, Nico Williams wakati wa majira ya joto. Lakini amejibu kwa njia bora zaidi.

Bao la Jumatano, lililoiweka Barca uongozini, lilikuwa la sita kwenye Ligi ya Mabingwa pekee hadi sasa msimu huu.

Katika mashindano yote, Raphinha amefunga mabao 27 na kusaidia mengine 23.

Kwa hivyo wakati winga huyo wa zamani wa Leeds United alipotolewa zikiwa zimesalia dakika 20 mpira kumalizika kulikuwa na wasiwasi uwenda akwa ameumia, lakini Flick ameondoa wasiwasi huo.

"Hajajeruhiwa. Amechoka tu," alisema bosi huyo akiwahakikishia mashabiki alipozungumza na waandishi wa habari.

Iwapo kutakuwa na matokeo mabaya wakati Wakatalunya hao wakijiandaa kumenyana na Leganes kwenye La Liga Jumapili bado haijaonekana.

Raphinha ameanza mechi zote isipokuwa moja kwenye mashindano yote kufikia sasa msimu huu, mechi yake pekee kama mchezaji wa akiba ilikuja katika kichapo cha kushangaza dhidi ya Osasuna Septemba.

Lakini kutokana na Leganes kuhangaika juu ya eneo la kushushwa daraja la La Liga, huenda ikafaa kufikiria mapumziko kutoka kwa kikosi cha kwanza, haswa wakati Ferran Torres alipotoka benchi dhidi ya Dortmund na kufunga mara mbili, na hatimaye kuamua mchezo huo kwa faida kwa Barcelona.

"Kuna mchezo mwingine Jumapili, na tutaona jinsi wachezaji wanavyopona," Flick aliongeza.

"Lakini benchi ni nzuri sana. Kila anayeingia lazima awe fiti asilimia 100."

# Mbappe nje ya dimba siku 10

**MADRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Kylian Mbappe atakuwa nje ya uwanja kwa siku 10 kutokana na jeraha la paja, vyanzo viliiambia ESPN Jana.

Fowadi huyo wa Ufaransa alibadilishwa dakika ya 35 katika mcherzo wa ushindi wa 3-2 Jumanne dhidi ya Atalanta kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kushukiwa kuwa na tatizo la paja la kushoto.

Hiyo inamaanishisha Mbappé atakosa pambano la LaLiga huko Rayo Vallecano leo Jumamosi.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Madrid haitamharakisha Mbappé kurejea kwa haraka kwani inaweza kuwa hatari ya kuzidisha jeraha la misuli.

"Kufuatia vipimo vilivyofanywa kwa Kylian Mbappé na idara ya matibabu ya Real Madrid, mchezaji huyo amegundulika kuwa na jeraha la paja katika mguu wake wa kushoto," taarifa ya klabu ilisema. „Maendeleo yake yatafuatiliwa."

Mbappé amefunga mabao 12 katika mechi 22 alizochezea Madrid katika michuano yote hadi sasa tangu ajiunge na klabu hiyo akiwa mchezaji huru msimu wa majira ya joto baada ya mkataba wake na Paris Saint-Germain kumalizika.

Licha ya kiwango chake cha kufunga, Mbappé amekabiliwa na ukosoaji kwa uchezaji wake huku Madrid ikipata vipigo vya hali ya juu katika msimu huu, hasa ikipoteza 4-0 nyumbani dhidi ya Barcelona.

Nahodha wa Real Madrid, Dani Carvajal ana imani Mbappé atabeba mataji kwa Los Blancos.

Carvajal, ambaye anauguza jeraha alisema kuhusu nyota huyo wa Ufaransa wakati akihudhuria hafla ya utoaji tuzo siku ya Jumatano: „Anabadilika vizuri sana. Amefunga mabao mengi na sisi licha ya ukosoaji aliopokea kwenye mchezo wake. Natumaini ataendelea hadi mechi mwisho wa msimu."

# Postecoglou akerwa na Werner

**GLASGOW, Scotland**

KOCHA mkuu wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou alitoa tathmini kali ya kwa Timo Werner katika sare ya 1-1 ya Ligi ya Europa dhidi ya Rangers siku ya Alhamisi, akisema uchezaji wa mshambuliaji huyo "haukubaliki."

Werner, ambaye anacheza katika msimu wake wa pili kwa mkopo Spurs kutoka RB Leipzig, nafasi yake ilichukuliwa na Dejan Kulusevski baada ya kuvumilia kipindi kigumu cha kwanza huko Ibrox.

Alipoulizwa ikiwa ubadilishaji huo ulifanywa kwa sababu za busara, Postecoglou alisema, "Ndio, hakuwa kwenye kiwango anachopaswa kuwa."

Spurs walikubali kufungwa ndani ya dakika mbili baada ya Kulusevski kuanzishwa, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Sweden akaifungia timu yake bao la kusawazisha.

"Nadhani Rangers walicheza vizuri sana. Tulijitahidi kidogo. 1-1, ndivyo ilivyo. Hatukucheza vyema vya kutosha kushinda mchezo," alisema Kulusevski baada ya mechi.

"Siku zote ni muhimu kufunga, lakini lazima tuanze kushinda michezo.

"Hatujashinda kwa wiki kadhaa. Kila mtu anahitaji kufanya zaidi kidogo kuliko tunavyofanya hivi sasa."


Postecoglou pia alirejelea uchezaji wa vijana wawili wa Spurs wenye umri wa miaka 18, Lucas Bergvall na Archie Gray.

Katika hali ya kukosekana kwa mabeki waandamizi wa Spurs -- Cristain Romero, Micky van de Ven na Ben Davies, Gray alijaza eneo la beki wa kati huko Glasgow na kupata sifa kutoka kwa kocha wake ambaye alimuelezea kama ni bora.

Bergvall alianzishwa kama sehemu ya ubadilishaji wa dakika ya 75 ambao ulionekana kuwa muhimu katika kusaidia Spurs kupata pointi muhimu.

Postecoglou, ambaye ameona jukumu lake kama kocha mkuu wa Spurs likiwa na shinikizo kubwa baada ya mfululizo wa matokeo yasiyoridhisha katika wiki za hivi karibuni, alidokeza mchango ulioletwa na vijana hao alipoulizwa kama anamhitaji Werner na wachezaji wengine waandamizi kutoa mchango mkubwa zaidi timu.

"Nadhani unapokuwa na umri wa miaka 18, nadhani haikubaliki kwangu. Nilimwambia Timo, ni mchezaji wa kimataifa wa Ujerumani."



# AMORIM AFURAHISHWA MZOZO WA HOJLUND, AMAD

**PLZEN, Czechia**

RUBEN Amorim amesema ilikuwa "ishara nzuri" kuona Rasmus Hojlund na Amad wakiwa kwenye mzozo mkali baada ya ushindi wa 2-1 dhidi ya FC Viktoria Plzen kwa sababu inaonesha kuwa wanajali.

Huo ulikuwa mchezo wa Ligi ya Europa uliopigwa juzi.

Hojlund alifunga mara mbili wakati United wakitoka nyuma kwa bao moja na kuandikisha ushindi wao wa kwanza ugenini Ulaya tangu kuifunga Real Betis Machi 2023.

Lakini mshambuliaji huyo wa Denmark na Amad ilibidi watenganishwe na Lisandro Martínez baada ya filimbi ya mwisho huku wawili hao wakishutumiana kwa kushindwa kuchukua pasi sahihi wakati wa dakika za lala salama.

"Kwangu mimi ni safi," alisema Amorim alipoulizwa kuhusu makabiliano hayo.

"Tunahitaji kuhisi kitu. Katika wakati huu, tunahitaji kuhisi kitu. Ikiwa tunahitaji kupigana ni kama familia. Kwangu mimi ni ishara nzuri sana. Tunahitaji kuhisi kitu na hiyo ni muhimu."

Alipoulizwa kama anapendelea wawili hao kuondoa tofauti zao kwa sababu inaonesha wanajali, Amorim alisema: „Hilo liko wazi, usipojali, hufanyi chochote. Unapojali, unapigana na kaka yako hata na baba yako na mama yako. Kwangu mimi ni ishara nzuri sana.

"Ni jambo la kawaida, ni jambo chanya, jambo la afya. Niliwaacha wachezaji na nahodha watulize mambo. Nikiona ni mengi sana nitaingia ndani ya chumba cha kubadilishia nguo. Lakini ni nafasi yao, wanapaswa kuzungumza."

United ilihitaji bao la ushindi dakika ya 88 kutoka kwa Højlund katika uwanja wa Doosan Arena baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kufuta bao la kwanza dakika sita tu baada ya kuingia kama mchezaji wa akiba kipindi cha pili.

"Nina furaha kwamba tumeshinda mchezo na bado tunapigana, hilo ni jambo zuri sana," alisema Amorim.

HABARI MICHEZO

# ELVIS RUPIA AFIKISHA MABAO SABA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Singida Black Stars raia wa Kenya, Elvis Rupia, ambaye anawaniwa na klabu ya Simba kwa ajili ya kumsajili kwenye dirisha dogo la usajili, juzi alifunga mabao mawili na kukaa juu ya kilele cha orodha ya wafungaji wa mabao mengi Ligi Kuu, akifikisha mabao saba.

Kwenye Uwanja wa Liti, Singida, straika huyo mwenye mbio na nguvu pamoja na mashuti makali, alifunga mabao yote mawili yaliyoiwezesha timu yake ya Singida Black Stars kushinda mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji.

Alipachika mabao hayo dakika ya nane, na 15, kabla ya Yassin Mgaza kuifungia Dodoma Jiji bao la kufutia machozi, dakika ya 58.

Mabao hayo yamemfanya sasa kuongoza kwenye ufungaji Ligi Kuu, akimpiku kinara wa muda mrefu, Selemani Mwalimu wa Fountain Gate aliyebakiwa na mabao sita.


Matokeo hayo yanaifanya Singida Black Stars kufikisha pointi 27 sawa na Yanga, lakini ikiendelea kuwa nafasi ya nne kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa huku Dodoma Jiji ikisalia na pointi 16, kwenye nafasi ya 10 kwenye msimamo.

Kaimu Kocha Mkuu wa Singida Black Stars, Ramadhan Nswanzurimo, alisema ilikuwa ni mechi nzuri na ya kimbinu.

"Ilikuwa mechi ya kimbinu, kocha mmoja akibadili mfumo mwingine anabadilika, kipindi cha kwanza tulitawala mchezo, cha pili hatukuwa vizuri kwa sababu wachezaji wangu walionekana kujiamini kupita kiasi, ilionekana kama wamechoka kimwili, muhimu tumepata pointi tatu, bado tuna kazi ya kufanya,“ alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Macky, Mexime, alisema waliiharibu mechi dakika 20 za mwanzo ambapo hawakuwa makini na kuweza kutoa mwanya kwa wapinzani wao kufunga mabao yote mawili.

"Mechi tuliiharibu dakika 20 za mwanzo, hatukuwa makini tukawapa mabao rahisi, makosa mawili wakayatumia, kipindi cha pili tukaamka usingizini tukaitawala mechi lakini tukapata bao moja tu. Niseme tu walituhukumu kutokana na ubora wa wachezaji wao,“ alisema.




Mwanafunzi wa kidato cha tatu katika shule ya sekondari Mtakatifu Theresa, Maria Mtega (kulia) akionyesha programu ya simu waliyoiunda na wanafunzi wenzake (pichani) kwenye tamasha la kuonyesha vipaji na ujuzi wa tehama jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Serikali yazitakia heri Simba, Yanga

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI kupitia kwa msemaji mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa imezitakia heri klabu za Simba na Yanga kwenye mechi zao za kimataifa zitakazochezwa mwishoni mwa wiki hii zifanye vizuri ili kusongambele kwenye michuano hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma baada ya makabidhiano ya Ofisi ya Msemaji Mkuu wa Serikali, Msigwa ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo alisema.

"Mwishoni mwa wiki kutakuwa na michezo ya kimataifa ya klabu ya Yanga na Simba nawatakia heri wafanye vizuri, wapate pointi na kujihakikishia safari ya kusonga mbele kwenye mashindano wanayoshiriki," alisema Msigwa.

Aidha, alisema kwenye Wizara kuna miradi mikubwa ya AFCON inakuja na kuomba waandishi wasaidie kuitangaza.

"Pia kwa sasa tuiandae nchi kwa ajili ya CHAN na AFCON ni matukio makubwa ambayo Wizara yetu inahusika, tunaomba ushirikiano wenu katika kutangaza,"alisema.

Tanzania itakuwa mwenyeji wa fainali za Afcon za mwaka 2027 pamoja na Kenya na Uganda na CHAN zitakazofanyika mwakani kwa kushirikiana na nchi za Uganda na Rwanda.

## Yanga kufa na TP Mazembe

INATOKA UK. 24

karibuni lakini bado wachezaji wameendelea kupambana kwenye mazoezi na wanaamini watafanya vizuri kwani timu ina wachezaji wengi waliocheza na TP Mazembe mwaka jana katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi.

"Tumepitia katika mazingira magumu kutokana na matokeo mabaya, lakini sisi kama wachezaji tumeendelea kupambana na mazoezi, tuliokuja kucheza ni kwa asilimia kubwa ni wale wale tuliocheza dhidi ya TP Mazembe kwenye Kombe la Shirikisho mwaka jana, tukashinda michezo yote miwili dhidi yao,“ alisema Ramovic.

Yanga iliifunga TP Mazembe mabao 3-1 katika mchezo wa kwanza uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Februari 19 mwaka jana, kabla ya kushinda tena kwenye uwanja watakaochezea leo bao 1-0, mchezo ukipigwa Aprili 2 mwaka jana.

TP Mazembe yenyewe ina pointi moja tu iliyoipata ilipocheza dhidi ya MC Alger kwa kutoka suluhu, hivyo nayo inahitaji pointi tatu ili kuweka hai matumaini ya kusonga mbele kwenye hatua inayofuata kwenye kundi hilo ambapo mechi nyingine ya kundi hilo kati ya MC Alger itakayokuwa nyumbani dhidi ya Al Hilal, itachezwa leo saa 4:00 usiku kwa saa za Tanzania.

## Fadlu: Tutashambulia mwanzo, mwisho

INATOKA UK. 24

hili,“ alisema Fadlu raia wa Afrika Kusini.

Simba inashika nafasi ya tatu kwenye kundi hilo linaloongozwa na CS Constantine yenye pointi sita, Blavo do Maquis ya Angola ikishika nafasi ya pili ikiwa na pointi tatu kama Simba iliyo chini kwa idadi ya mabao ya kufunga, huku CS Sfaxien ikiburuza mkia, ikiwa haina pointi yoyote.

Katika mchezo wa kwanza, Simba iliifunga Bravo do Maquis ya Angola bao 1-0, kabla ya Jumapili iliyopita kufungwa ugenini nchini Algeria mabao 2-1 dhidi ya CS Constantine.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, amesema kama timu hiyo imefungwa na timu mbili zilizo kwenye kundi hilo, moja ikiwa nyumbani kwao, basi hakuna namna yoyote wao washindwe kupata pointi tatu kutoka kwao.

"Itakuwa haina maana yoyote, yaani timu imefungwa kwao, halafu imepoteza mechi nyingine ugenini inakuja kucheza na timu ambayo tunajinasibu kuwa tunataka kwenda robo fainali halafu tushindwe kuchukua pointi tatu itakuwa si sawa. Kama Simba tunaitaka robo ni lazima na sisi tuchukue pointi tatu kwao ,“ alisema Ahmed.

# Michezo

Nipashe

Jumamosi Desemba 14, 2024


## Raphinha awatoa hofu Barca

UKURASA 21





Kiungo wa Azam FC, Djibril Sylla (kushoto) akimtoka beki wa Tabora United katika mchezo wa Ligi Kuu uliochezwa jana kwenye uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora, wenyeji Tabora United walishinda mabao 2-1**. PICHA: AZAM**

# YANGA KUFA NA TP MAZEMBE LEO

●●●Kocha Ramovic amesema watafanya kila njia kuhakikisha wanapata ushindi kwa kuwa....

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema watafanya kila njia kuhakikisha wanapata ushindi wa ugenini leo dhidi ya TP Mazembe ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kuwa na matumaini ya kuingia hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kutoka Kundi A.

Yanga leo itashuka ugenini, Uwanja wa Mazembe, Lubumbashi, saa 10:00 jioni kucheza mchezo wa raundi ya tatu ambapo inahitaji ushindi kwa udi na uvumba ili kurejesha matumaini ya kuelekea kwenye robo fainali ya michuano hiyo.

Ramovic, amesema ameshaandaa mfumo wa kucheza mchezo wa leo na anaamini wachezaji wake watautekeleza kwa vitendo wakiwa ndani ya uwanja.

"Tunacheza na timu ngumu, inayocheza soka la moja kwa moja. Tutajitahidi kumiliki mechi, lakini kuna wakati tutapoteza mipira nimeshatengeneza mfumo unaotuelekeza nini tutafanya ili kuinyang'anya haraka na hii ni kazi ya timu nzima kurudi nyuma na kusaka mpira miguuni mwa wapinzani na kushambulia kwa kasi, naamini tunakwenda kufanya vizuri," alisema kocha huyo.

Yanga inacheza mechi ya leo ikiwa haina pointi yoyote, ikiwa imecheza mechi mbili na kupoteza zote kwa mabao 2-0, dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan na MC Alger ya Algeria.

Kiungo mshambuliaji wa timu hiyo ambaye wakati mwingine hucheza kama winga, Maxi Nzengeli, amesema pamoja na kwamba wamepitia kwenye mazingira magumu ya kupoteza mechi kwa siku za

INAENDELEA UK. 23

## Kocha Fadlu: Tutashambulia mwanzo, mwisho

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba Fadlu Davids, amesema kwenye mchezo wa kesho dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia, watacheza kwa kushambulia muda wote wa mchezo kwa kuwa hakuna kingine kinachotakiwa zaidi ya ushindi.

Akizungumza kuelekea kwenye mchezo huo wa raundi ya tatu, Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi dhidi ya timu hiyo ya Tunisia, kocha huyo alisema haijalishi watachezaje, kama watacheza soka safi au vinginevyo, lakini kinachotakiwa ni kupata ushindi kwenye mchezo huo kwa njia yoyote ili kuendeleza rekodi ya kuzoa pointi tatu nyumbani ambazo zinaweza kuwasaidia kuvuka hatua ya makundi na kwenda robo fainali.

"Tunachohitaji ni ushindi tu, haijalishi tumecheza vipi, tumecheza vizuri zaidi kuliko wenzetu CS Constantine Jumapili iliyopita tukiwa ugenini, lakini wenzetu walitumia makosa yetu madogo kutuadhibu na wakashinda mechi, na sisi tunataka kupata ushindi kwenye mchezo utakaochezwa nyumbani mbele ya mashabiki wetu ambao watakuja wengi kutushangilia," alisema Fadlu.

Alisema kwa mahesabu ambayo wameyapiga, wana uwezo wa kuliongoza Kundi A, au kushika nafasi ya pili nafasi ambazo zitawasaidia kusonga mbele.

"Tukishinda tutafikisha pointi sita, na tutakuwa tumebakisha michezo mitatu ambayo kwa vyovyote hatuwezi kucheza yote bila kupata pointi tatu au nne katika ya mechi hizo, na kimahesabu ukishakuwa na pointi tisa au kumi utakuwa umeshavuka kundi," alisema.

Kutokana na hilo, alisema katika mchezo wa kesho amewataka wachezaji wake kushambulia muda mwingi wa mchezo na kutumia kila nafasi itakayopatikana ili kupata mabao yatakayowawezesha kuzoa pointi tatu.

"Tunataji mabao, ikiwezekana mengi zaidi ambayo yanaweza kutusaidia mbele ya safari kama tutakuwa tumefungana pointi na wenzetu mwishoni mwa michezo ya kundi

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >